# Nipashe

Jumamosi Novemba 23, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580083

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13



## Asimulia alivyotaka kuwakimbia mapacha wanne njiti hospitalini

UKURASA 3

# Adaiwa kuficha kadi 23 za ATM sehemu za siri

• **Polisi** wasema alikuwa akizitumia kufanyia wizi wa kimafia baada ya kuwatapeli wastaafu... *Endelea uk. 2*



## Rais aonya utapeli wa fidia



UKURASA 2




UKURASA 2

Majeneza yenye miili ya madaktari watatu wanaofanya kazi katika Kituo cha Afya cha Kabuku na Kituo cha Afya Mkata, wilayani Handeni, mkoani Tanga, ambao walifariki dunia kwa ajali ya gari usiku wa kuamkia jana, katika kijiji cha Taula, Kata ya Kwedizinga, wakati wakitoka Moshi mkoani Kilimanjaro kikazi, wakati wa shughuli ya kuaga iliyofanyika katika Kituo cha Afya cha Mkata jana. **PICHA: STEVEN WILILIAM**

# Madaktari watatu wafariki wakitoka mafunzoni KCMC




Scan Hapa

Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** SIMBA SC, RUVU SHOOTING NI VITA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM aonya utapeli wa madai ya fidia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amewaonya wananchi kutotumia fursa ya makao makuu Dodoma kuwa chanzo cha kufanya utapeli kwa kutengeneza madai ya uongo ili walipwe fidia.

Magufuli alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wananchi baada ya kuweka jiwe la msingi kwenye mradi wa ujenzi wa kituo cha mabasi, soko la kisasa, ujenzi wa nyumba za askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) na ujenzi wa hospitali ya Uhuru iliyoko Wilaya ya Chamwino.

Alisema Dodoma kuwa makao makuu kusifanywe kama chanzo cha kuitapeli serikali bali watu wadai maeneo yanayostahili.

Alibainisha kuwa kuna watu wanafikiri hatua hiyo ni sehemu ya kutengeneza fedha za bure za serikali.

"Wanajidanganya sana kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Vijiji Na. 5, ardhi ya mtu ikichukuliwa ni lazima alipwe fidia lakini ardhi ya mtu ikichukuliwa si asili yake hawezi kulipwa fidia kwa kuwa alivamia anatakiwa kuilipa fidia serikali," alisema.

Rais alisema nyumba zilizopo eneo la Kisasa jijini Dodoma ameshiriki kuzijenga na watu wote katika nyumba hizo 300 walilipwa fidia.

"Kuna baadhi ya viwanja vya serikali vilipotea kwa watu binafsi na wapo viongozi wa serikali walijibinafsisha viwanja ambavyo ni mali ya serikali, ukisikia leo mtu anajitokeza anasema anadai fidia kwenye nyumba za kisasa unamshangaa kwa sababu mimi nafahamu tulilipa zote, na nyaraka zilisainiwa hadi kwa Mkuu wa Mkoa kwa wakati ule," alisema.

Magufuli alisema katika eneo la kituo cha mabasi, soko na nyumba za askari akijitokeza mtu kudai fidia lazima amshangae.

"Kwa sababu eneo hili lilikuwa mali ya serikali na lilikuwa eneo la polisi walikuwa wakifanya mazoezi ya bunduki zao, sasa yeye alikuwa anakaa humo na bunduki zinapigwa, wakati nyani nao walikimbia," alisema.

Rais Magufuli alisema isifike mahali kila eneo mtu anasema ni lake watambue kuwa serikali ilikuwapo.

"Wapo kweli wachache kule Chamwino wanadai waliokuwa wamebaki, lakini asilimia zaidi ya 90 wamelipwa fidia

INAENDELEA UK.7

# Adaiwa kuficha kadi 23 za ATM sehemu za siri

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linamshikilia Halima Juma (23), mkazi wa Chalinze mkoani Pwani, baada ya kudaiwa kukutwa na kadi za ATM 23 alizozificha sehemu za siri.

Imedaiwa na jeshi hilo kuwa alikuwa anazitumia kuiba fedha katika benki mbalimbali nchini kwa kujitolea kuwapa msaada watu wasiojua kutumia kadi za ATM, baadaye kuwabadilishia kadi zao kinyemela.

Kamanda wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, alidai mbele ya waandishi wa habari jijini jana kuwa, mtuhumiwa huyo alikamatwa Jumanne kwenye tawi la Benki ya CRDB Mbagala wilayani Temeke.

"Askari wetu walimtilia shaka binti huyu ambaye wakati huo alikuwa katika chumba cha ATM cha CRDB akijifanya anawasaidia wazee na wastaafu wasiojua kutumia mashine hizo.

"Lengo lake lilikuwa ni kuchukua namba za siri zao kisha kuwabadilishia kadi za ATM na baadaye kuwaibia fedha kwenye akaunti zao kwa kutumia kadi halisi za wahusika baada ya kuzibadilisha 'password' (nywila)," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na askari wanaolinda benki hiyo na alipopekuliwa katika pochi yake aliyoificha sehemu za siri, alikutwa na kadi za ATM 23 za watu mbalimbali.

"Alikutwa na kadi saba za CRDB, sita za NMB na benki za NBC, Amana na Posta, ambazo alikutwa na kadi mbili mbili kwa hizo benki zingine. Pia alikutwa na kadi moja moja za benki za ACB, Stanbic, DTB na Equity," alidai.

Kamanda Mambosasa alidai mtuhumiwa huyo anaendelea kuhojiwa na jeshi hilo na atafikishwa mahakamani wakati wowote.

Katika hatua nyingine, Kamanda Mombasasa alisema jeshi limejipanga kuhakikisha uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika kesho nchini, unafanyika kwa amani na utulivu.

Alitoa onyo kwa mtu yeyote au kikundi kitakachojaribu kuvuruga amani kuwa jeshi hilo halitasita kukichukulia hatua za sheria.

Kamanda Mambosasa pia aliwataka wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kuwa na tahadhari ya mvua inayoendelea kunyesha, akikumbusha kuwa kumekuwa kukitokea maafa kutokana na mafuriko jijini.




Rais John Magufuli akiwa pamoja na viongozi wengine akivuta utepe kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa stendi kuu ya mabasi, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Madaktari watatu wafariki wakitoka mafunzoni KCMC

**Na Steven William,** MUHEZA

MADAKTARI watatu wa vituo vya afya Kabuku na Mkata wilayani Handeni mkoani Tanga, wamefariki dunia baada ya lori walilopanda kutoka mafunzoni KCMC mkoani Kilimanjaro kupata ajali.

Ajali hiyo iliyotokea usiku wa kuamkia jana katika Kijiji cha Taule, Kata ya Kwedizinga wilayani Handeni, imesababisha vifo vya madaktari Razaro Mpiziwa, Lucas Lubacha na Mussa Muro.

Miili ya madaktari hao iliagwa jana katika Kituo cha Afya Mkata wilayani humo kabla ya kusafirishwa kwenda mikoa wanakokotoka.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigella, aliongoza viongozi na wananchi kuaga miili hiyo, akieleza kuwa madaktari hao walikuwa wakitokea mkoani Kilimanjaro walikoshiriki mafunzo ya kutumia vifaa vya kisasa katika kupima magonjwa ya tumbo. Mafunzo yalitolewa katika Hospitali ya KCMC. Shigella alisema vifo vya madaktari hao vimewasikitisha kwa kuwa serikali imepoteza nguvu kazi ya taifa na watazidi kukumbuka mchango wao.

Mbunge wa Muheza, Balozi Adadi Rajabu, alisema ameshtushwa na taarifa za vifo vya madaktari hao, akieleza kuwa ni pigo kwa serikali.

Akizungumzia ajali hiyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alidai madaktari hao walikuwa wanatoka KCMC mjini Moshi walikokuwa wanashiriki semina kuhusu matumizi ya vifaa vya kitabibu.

Alieleza kuwa wakati wanarudi kwenye vituo vyao vya kazi, walipanda basi lililokuwa linakwenda Tanga mjini wakiwa madaktari wanne, lakini mmoja alishuka wilayani Korogwe.

Alidai kuwa walipofika Segera, madaktari hao watatu walishuka kwenye basi hilo na kulazimika kupanda lori la mizigo aina ya Volvo ili wafike Kabuku na mji mdogo wa Mkata.

"Bahati mbaya lori hilo lilipofika katika eneo la Kijiji cha Taule, Kata ya Kwedizinga wilayani Handeni, lilipata ajali kwa kutumbukia katika bonde na hatimaye watu wanne ambao walikuwa wamepanda katika lori hilo walifariki dunia wakiwamo madaktari watatu na utingo wa lori hilo ambaye hajafahamika jina lake mara moja.

"Dereva wa lori hilo amejeruhiwa na amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa, Bombo mjini Tanga," alisema Kamanda Bukombe.



Magari na Bajaj yakipita kwa tabu kwenye dimbwi la maji ya mvua katika eneo la Best Bite Namanga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Asimulia alivyotaka kuwakimbia mapacha wanne njiti hospitalini

**Na Romana Mallya**

OFISA Tarafa ya Kibamba, Ubungo jijini Dar es Salaam, Beatrice Mbawala, amesimulia changamoto alizopata baada ya kujifungua watoto mapacha wanne njiti, ambao gharama za kuwatunza hadi kufikia hatua nzuri ya ukuaji ilifikia Sh. milioni 100.

Mbawala ni miongoni mwa wazazi waliofika jana katika Hospitali ya Aga Khan kusherehekea Siku ya Mtoto Njiti Duniani ambayo kila mwaka huadhimishwa Novemba 17, mwaka huu.

Akizungumza jana katika sherehe hizo ambazo zililenga kuelimisha namna ya kuwalea watoto hao ambao wana changamoto kubwa ya malezi, Mbawala alisema mara ya kwanza alipowaona alipata wasiwasi kuhusu namna atakavyowatunza.

Alisema hakuwahi kuwashuhudia watoto wadogo kama hao ambao ukubwa wao ulikuwa sawa na simu ya kiganjani.

Alisema alijifungua mtoto wake wa kwanza wa kike mwaka 2015 bila tatizo lakini ilipofika Januari 29, mwaka 2017, ndipo alipojifungua watoto wanne mapacha wa kiume wawili na wa kike wawili.

Mbawala alisema kabla ya kujifungua watoto hao, alipata uchungu na alipofika hospitalini aliambiwa kwamba atafanyiwa upasuaji ili kumwokoa yeye na watoto.

"Nilifanyiwa upasuaji wa dharura, wakati madaktari wanapita wodini waliniambia kwamba kwa uzoefu walionao, watoto niliojifungua ni wakubwa, kwa hiyo picha iliyojengeka kichwani na nilichokwenda kukiona siku mbili baada ya kujifungua kilikuwa tofauti," alisema.

Mama huyo alisema alipokwenda kuwaangalia siku ya pili baada ya kujifungua, alishangaa kuwaona wakiwa na ukubwa sawa na simu ya mkononi.

INAENDELEA UK. 8

# Magufuli ashusha neema Polisi

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

RAIS John Magufuli ameagiza jengo lililokuwa la Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) kuwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, huku akiwataka askari kujiepusha na vitendo vya rushwa na kubambikia watu kesi kwani ni vitu vinavyochafua taswira ya jeshi hilo.

Magufuli alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akiweka jiwe la msingi katika ujenzi wa nyumba 118 za Polisi wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia(FFU).

Alisema amefurahishwa na hatua ya Jeshi la Polisi kuhamia Dodoma na kwamba amewapa jengo hilo kwa sababu ya kufurahishwa na kazi kubwa wanayofanya ya kulinda amani na usalama wa nchi.

"Nimefurahi kusikia mmehamia Dodoma maana ningeshangaa sana kama mimi nimehamia wewe IGP upo huko, usingefanya hivyo ningeteua IGP wangu wa hapa Dodoma," alisema Rais Magufuli.

"Kwa kuwa mmeamua kufanya hivyo, askari huwa hasubiri nyumba nimeamua kuwapa zawadi ya jengo moja kubwa lenye ghorofa nne ambalo lilikuwa linatumiwa na Ruwasa sasa itakuwa makao makuu ya polisi," alisema.

Alimtaka Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Giles Muroto, arudi kwenye ofisi yake iliyokuwa imechukuliwa kwa ajili ya kuwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.

Rais Magufuli pia alilitaka Jeshi la Polisi kujiepusha na vitendo vinavyodhalilisha jeshi hilo kwa kuomba rushwa na kubambikizia watu kesi.

"Wananchi toeni ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa kufichua wahalifu na endapo wananchi mtatoa ushirikiano usalama wa raia utaimarika hapa nchini," alisema.

Aidha, alisema utaratibu wa kutumia nguvu kazi ya serikali (force account) wataweza kujengwa nyumba 400 kwa kutumia Sh. bilioni 10 na kwamba wangetumia makandarasi binafsi wasingeweza kujenga kwa gharama hiyo.

"Wangetumia utaratibu wa kutangaza zabuni isingewezekana kujenga nyumba 400, utaratibu huu umeleta tija kubwa kwa serikali, tumefanikiwa kujenga vituo vya afya 352 kwa gharama Sh. bilioni 182 na kama wangetumia utaratibu wa zabuni zingetumika Sh. trilioni moja pia tumejenga majengo ya wizara mji mkuu wa serikali kwa utaratibu huu," alisema.

Alipongeza jeshi hilo kwa kupunguza matukio ya uhalifu wa kutumia silaha.

"Nalipongeza Jeshi la Polisi na

INAENDELEA UK. 8

# MOI sasa yajivunia matibabu ya kibingwa

**Na Beatrice Moses**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) imeelezea mafanikio yake katika kutoa huduma za matibabu kwa wananchi baada ya serikali ya awamu ya tano kuwekeza kwenye miundombinu, vifaa tiba na dawa katika kipindi cha miaka minne.

Imesema kwa sasa hakuna mgonjwa anayelala chini kama ilivyokuwa miaka kadhaa iliyopita kwa kuwa vitanda kwa wagonjwa wa kawaida vimeongezwa kutoka 150 hadi 340.

Aidha, imesema katika kuboresha huduma za upasuaji wa ubongo, serikali imetoa Sh. bilioni 7.9 kwa ajili ya ujezi wa maabara ya kisasa ya upasuaji huo ambao kwa kitaalamu unajulikana kama Endovascula Neuro-suite.

Hayo yamebainishwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya taasisi hiyo katika miaka minne ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

Dk. Boniface alisema ujenzi wa maabara hiyo ya kisasa inayotarajiwa kuanza kufanya kazi Januari, mwakani, utaifanya Tanzania kuwa kivutio cha matibabu kwa kuwa ni ya kwanza kwa Afrika Mashariki na ni miongoni mwa nchi chache Afrika zinazotoa huduma za upasuaji wa ubongo bila kufumua fuvu.

Alisema maboresho mengine yamefanywa kwa kuongeza vyumba vya upasuaji kutoka sita hadi tisa, hatua ambayo imesaidia kuongeza kasi ya kutibu, hivyo imewavutia wagonjwa kwenda kutibiwa katika taasisi hiyo.

Hatua hiyo, alisema imeongeza idadi ya wagonjwa wanaokwenda kwa upasuaji kutoka 500 hadi 700 kwa mwezi ndani ya miaka hiyo minne na wagonjwa 43,200 wamefanyiwa upasuaji mbalimbali.

Alisema baada ya kuingia madarakani, Rais John Magufuli alipotembelea wodi za MOI, alikuta kuna changamoto ikiwamo wagonjwa kulazwa sakafuni kutokana na uhaba wa vitanda.

"Siyo hivyo tu pia kulikuwa na uhaba wa vifaa tiba na dawa, vifaa vya uchunguzi na wagonjwa wengi walilazimika kusubiri huduma kwa muda mrefu kwa kuwa vyumba vya

INAENDELEA UK. 8


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC** tutauza kwa **MNADA WA HADHARA,** dhamana za wadaiwa. Mnada utafanyika kuanzia saa **4:00 asubuhi** na kuendelea mahali dhamana zilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

| No | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | TAREHE YA MNADA | BRANCH |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MIRAJI SAIDI MDOE | Nyumba ya makazi iliyopo Wazo, yenye leseni ya mauziano. | 06/12/2019 | TEGETA |
| 2 | JOHN DAUDI LINYAWA | Nyumba ya makazi iliyopo Kunduchi Mtongani yenye hati ya mauziano. | 04/12/2019 | TEGETA |
| 3 | MWANAHAMHISI MBEGU ATHUMANI | Nyumba ya makazi iliyopo Kunduchi Mtongani yenye hati ya mauziano. | 04/12 /2019 | KIJITONYAMA |
| 4 | ONESMO PETER MASIMA | Nyumba ya makazi iliyopo Ukonga Mazizini. | 07/12/2019 | UKONGA |
| 5 | JAMILA KONDO GEMA | Nyumba yenye leseni ya makazi na. ILA028172. Iliyopo eneo la Kipunguni. | 07/12/2019 | UKONGA |
| 6 | SALUM KONDO MWINYIMKUU | Nyumba yenye leseni ya makazi na. KND006783. Iliyopo eneo la Tandale. | 11/12/2019 | TANDALE |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537

**AU**

Mkurugezi Mtendaji
Akiba Commercial Bank PLC,
P.O. BOX 699,
DAR ES SALAAM.
Tel: +255 022 211 8340-3

# Kigogo wizara ahukumiwa kifungo cha miaka 42 jela

**Na Hellen Mwango**

NAIBU Mkurugenzi wa Mazingira na Afya wa Wizara ya Afya, Elias Chinamo, amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni saba au kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 42 baada ya kupatikana na hatia katika mashtaka 14 ya kuomba na kupokea rushwa.

Mahakama hiyo pia imemwamuru kigogo huyo kulipa fidia ya Sh. milioni 18 anazodaiwa kuomba rushwa.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustina Mmbando, aliyesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam.

"Mahakama hii inakutia hatiani kwa makosa 14 ya kupokea rushwa na inakuhukumu kulipa faini ya Sh. 500,000 kwa kila kosa au kwenda jela miaka mitatu kwa kila kosa," alisema Hakimu Mmbando.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alifanikiwa kulipa faini hiyo ya Sh. milioni saba.

Katika kesi ya msingi, Chinamo alikuwa akikabiliwa na mashtaka 28, yakiwamo 14 ya kuomba na kupokea rushwa na makosa mengine 14 ya wizi.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai.

Swai aliita mashahidi wanane na kuwasilisha vielelezo sita kuthibitisha kesi ya Jamhuri.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa, kati ya mwaka 2011 na 2012, jijini Dar es Salaam, katika Benki ya CRDB, Tawi la Holland na NBC, Tawi la Kichwele, Chinamo alijipatia Sh. milioni 18 kwa manufaa yake binafsi kupitia akaunti zake zilizoko katika matawi ya benki hizo.

Ilidaiwa alijipatia fedha hizo kutoka kwa watu mbalimbali akiwamo Anyitike Kitalima, Joseph Bilago, Emanuela Safari, Fadhili Kinemile na Suzana Mchala ili kuwapa nafasi nyingine ya kuratibu semina na warsha mbalimbali, jambo ambalo lilikuwa chini ya mamlaka ya mwajiri wake.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na waumini baada ya Sala ya Ijumaa, kwenye Msikiti wa Gaddafi, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Wakatisha masomo wakihofia mto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Itwangi wilayani Shinyanga, wanalazimika kutohudhuria shuleni kipindi cha mvua wakihofu kusombwa na maji ya mto ambao ni lazima wauvuke kabla ya kuifikia shule hiyo.

Imeelezwa kuwa wanafunzi wanaoishi katika Kijiji cha Igembya ndiyo waathirika zaidi wa adha hiyo kutokana na kuvunjika kwa daraja lililokuwapo.

Hayo yalibainishwa juzi na mmoja wa wazazi wa kijiji hicho, Fuli Shija, kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Solwa, Ahmed Salum.

Mbunge huyo aliitisha mkutano huo ili kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi sambamba na kuwanadi wagombea wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wanaotokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Shija alimwomba mbunge huyo kuitatua kero hiyo kwa kujenga daraja ili watoto wao wasiendelee kukosa masomo kwa hofu ya maji ya mto.

"Tunashukuru mbunge kwa kututembelea kwenye kijiji chetu, tuna kero kubwa mheshimiwa tunaomba ututatulie, kuna daraja la kutuunganisha na kijiji jirani cha Itwangi, watoto wetu husoma shule ya sekondari huyo, limeshasombwa na maji na mvua kubwa ikinyesha, hushindwa kwenda shule," alisema.

Diwani wa Nyida wilayani humo, Selemani Segereti, alikiri daraja hilo kuharibika na kueleza kuwa tayari walishafanya tathmini kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (Tarura) na kubaini zinahitajika Sh. milioni 20.

Alisema kinachochelewesha kwa sasa ni wakala hao kusubiri fedha za matengenezo ya barabara kutoka serikalini, hivyo akamwomba mbunge wao huyo kuongeza nguvu ili daraja hilo lijengwe haraka kabla halijaleta madhara ya vifo.

Mbunge wa Solwa (Salum) aliwatoa wasiwasi wananchi hao kuwa suala hilo atalishughulikia haraka na kutoa wito kwa wanafunzi na wananchi, kutojaribu kuvuka mto wakikuta maji yamejaa.

# Wenye viwanda wapatiwa elimu ya ubora wa bidhaa

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limewapatia elimu wenye viwanda vinavyozalisha bidhaa ambazo hazijathibitishwa ubora mkoani Singida, hatua ambayo itawasaidia kuunga mkono juhudi za serikali za ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Elimu hiyo ambayo imepokewa kwa mwitikio mkubwa na wenye viwanda mkoani hapa, ilianza kutolewa na maofisa wa shirika hilo kuanzia Novemba 11, mwaka huu na inatarajiwa kuhitimishwa keshokutwa.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa jana, Mkaguzi wa Shirika hilo, Domisiano Rutahala, alisema kwa muda wa siku 16 wamekuwa wakitoa elimu kuhusu umuhimu wa bidhaa zinazozalishwa kupata alama ya ubora kwa wenye viwanda vya kukamua mafuta ya alizeti na kuzalisha unga wa mahindi.

"Maofisa wa shirika letu tupo hapa kwa ajili ya kuwafikia wenye viwanda na wazalishaji ambao bidhaa zao hazijathibitishwa kupata elimu, kuwasikiliza na kuwasaidia kufikia viwango," alisema Rutahala na kuongeza;

"Wenye viwanda wamefurahi kuona tunawafuata hadi mlangoni, wamepokea elimu kwa mwitikio mzuri na wameahidi kutumia elimu waliyoipata kuwa mabalozi wazuri kwa wenzao ili nao wajitokeze kuthibitisha ubora wa bidhaa zao," alisema.

Rutalala alisema elimu hiyo ilikwenda sambamba na ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka ya kuuza vipodozi na kufanikiwa kukamata vipodozi vyenye viambata vya sumu, ambavyo vimepigwa marufuku kutokana na kuwa na madhara kwa binadamu.

Kwa mujibu wa Rutalala, mpango huo wa kuwapatia elimu wenye viwanda ambao wanazalisha bidhaa ambazo hazina ubora umeanzia mkoani Singida. Alitaja maeneo ambayo elimu hiyo ilitolewa kuwa ni Singida Manispaa, Kiomboi, Shelui, Mkalama na Manyoni

"Suala hili litaendelea na Halmashauri ya Itigi," alifafanua na kuongeza kuwa kutokana na kuguswa na elimu hiyo, wenye viwanda wengine walianza mara moja kutuma maombi kwenye shirika hilo kwa ajili ya bidhaa zao kuthibitishwa ubora.

Kuhusu ukaguzi kwenye maduka ya vipodozi, Rutahala alisema walifanikiwa kukamata vipodozi vyenye viambata sumu ambavyo vimepigwa marufuku kutokana na kuwa na madhara kwa watumiaji.

Vipodozi hivyo vinaondolewa kwenye soko kutokana na kuwa na madhara mbalimbali kwa watumiaji.

Baadhi ya madhara ya vipodozi hivyo ni kusababisha saratani ya ngozi, kupunguza kinga ya ngozi na kuathiri mfumo wa homoni za mwili, hivyo Rutalala aliwashauri watumiaji kuacha kutumia vipodozi vilivyopigwa marufuku.

# Wizara yajivunia kudhibiti viashiria hatarishi uchumi

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Viwanda na Biashara imesema katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, imefanikiwa kudhibiti mianya ya viashiria hatarishi vya uchumi na maendeleo nchini. Kamishna wa Vipimo wa wizara hiyo, Dk. Ludovick Christian, aliyasema hayo jana mjini Bagamoyo mkoani Pwani wakati akifungua kongamano la pili la Taasisi ya Kudhibiti Viashiria vya Vihatarishi vya Uchumi na Maendeleo Tanzania (IRMT), lililowakutanisha wadau kutoka sekta ya umma na binafsi.

Alisema moja ya viashiria ambavyo serikali imefanikiwa kuvidhibiti kwa kipindi hicho cha miaka minne ni pamoja na matumizi mabovu ya fedha za umma na usimamizi mbaya wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na shughuli nyingine zinazohusiana na jamii. Alisema katika kufikia malengo ya uchumi wa viwanda, kuna umuhimu wa kuendelea kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma na usimamizi bora wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali.

"Sasa hivi, tunaenda kwenye uchumi wa viwanda, ambao una mambo mengi ambayo yanatakiwa yaangaliwe kwa ufanisi zaidi. Na moja ya vitu vinavyotakiwa visimamiwe kwa ufanisi zaidi ni viashiria vya kuleta matokeo hasi katika utekelezaji wa majukumu," alisema. Dk. Christian alisema kutokana na mabadiliko ya teknolojia, kuna uwezekano mkubwa wa kuwapo kwa viashiria hivyo kwa sababu watu wanabuni mbinu mbalimbali kwa nia ovu ya kuufanya uchumi udorore. "Kwa sababu ya mabadiliko ya teknolojia, hata viashiria vya kuleta athari katika maendeleo ya uchumi navyo vinakuwa vingi. Kwa hiyo, bila kuwa na uangalifu wa kudhibiti matumizi ya fedha za umma, tutakwama kufikia malengo yetu tuliyojiwekea katika upande wa serikali na hata sekta binafsi," alisema.

Rais wa IRMT, Pius Maneno, alisema wamejipanga kutumia teknolojia kuvitambua vihatarishi hivyo na kuvidhibiti kabla havijasababisha madhara.

"Kazi hii ilianza muda mrefu kwa sekta ya binafsi na kwa sasa imefika pia kwa taasisi za serikali na tumeona matokeo mazuri sana na itasaidia kufikia malengo yetu kiuchumi, kikubwa zaidi ni kuendelea kuvitambua, na tunasisitiza matumizi ya teknolojia katika udhibiti wake," alisema.

Katibu Mtendaji wa IRMT, Fredrick Mgaya, alisema tangu taasisi hiyo ianzishwe, imesaidia kutoa mafunzo kwa mashirika ya umma na binafsi na imezalisha wataalamu 76 na kutengeneza mifumo ya ndani ya kudhibiti viashiria hivyo.



Mwakilishi kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Kitengo cha Dawati la Jinsia na Watoto, SSP Faidha Suleiman, akitoa mada jijini Dar es Salaam juzi, kwenye warsha ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuhusu ukatili wa kijinsia, iliyoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA), Tanzania. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waziri ataka kulipwa deni la bil. 2/- ardhi

**Na Munir Shemweta,** KILOMBERO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro kuzifuatilia taasisi za serikali zinazodaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.9 za kodi ya pango la ardhi.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo jana alipokutana na uongozi wa wilaya ya Kilombero na watendaji wa ardhi katika halmashauri hiyo na ile ya Mji wa Ifakara wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi.

Agizo hilo lilitokana na maelezo ya kuelezwa na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Stephano Kaliwa, kuwa miongoni mwa wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi katika halmashauri yake ni taasisi za serikali zinazodaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.9.

Alizitaja taasisi hizo kuwa ni Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) linalodaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.7 katika maeneo yake inayomiliki ya Kidatu, Kihansi na Mlimba na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) lilinalodaiwa Sh. 12,819,550.

Ofisa Mipango Miji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, Remigi Lipiki, alimweleza Naibu Waziri Mabula kuwa Tanesco imetaka kufanyika uhakiki kwanza wa deni lake kwa madai kuwa baadhi ya maeneo inayomiliki yalishachukuliwa na taasisi zingine ikiwamo Kidatu.

Dk. Mabula alisema halmashauri hiyo lazima ihakikishe inazifuatilia taasisi hizo ili zilipe madeni ya kodi ya ardhi kwa kuwa zimekuwa zikitenga fedha kwa ajili ya malipo ya huduma mbalimbali ikiwamo kodi hiyo ya pango la ardhi.

"Taasisi zinashindwa kulipa madeni na hazijachukuliwa hatua, haiwezekani deni lifikie zaidi ya Sh. bilioni moja. Fuatilieni suala hili na mchukue hatua za kisheria," alisema.

Mkurugenzi huyo alieleza changamoto kubwa inayoikabili halmashauri yake kuwa ni ukusanyaji kodi ya pango la ardhi kwa baadhi ya wawekezaji wa mashamba kutokana na kutokamilika taratibu za uhaulishaji mashamba hayo ambayo wamiliki wake hawana nyaraka.

Aliataja baadhi ya wamiliki wa mashamba hayo kuwa, ni Mufindi Paper Mills yenye hekta 10,000, Green Resource Limited hekta 25,000, Hiragro Ltd hekta 1,500 na Sygen yenye ekari 30,000.

Kwa mujibu wa Kaliwa, kutokana na kutokamilika mchakato wa uhaulishaji wa mashamba hayo kumekuwa na upotevu wa makusanyo ya kodi ya jumla ya Sh. 132,865,031 kila mwaka.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilimanjaro Queens inaweza, tujitokeze Chamazi kuishangilia

**TIMU** ya Taifa ya Tanzania Bara ya Wanawake, Kilimanjaro Queens, itashuka dimbani leo kuivaa Uganda kwenye mechi ya nusu fainali ya michuano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge Cup) kwa Wanawake inayofanyika katika Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam.

Kilimanjaro Queens, imefanikiwa kutinga hatua hiyo baada ya kushinda mechi zake zote za Kundi A, ambapo ilianza kwa kuichapa Sudan Kusini mabao 9-0 kisha ikatoa kipigo cha 4-0 dhidi ya Burundi kabla ya kuhitimisha kwa kuwatandika ndugu zao wa Tanzania Visiwani, Zanzibar Queens kwa mabao 7-0.

Hivyo, Kilimanjaro Queens itaivaa Uganda ikiwa haijapoteza mechi hata moja wala kuruhusu nyavu zao kutobolewa kwenye michuano hiyo, ambayo inawania kulitwaa taji hilo kwa mara ya tatu mfululizo.

Lakini inakutana na Uganda ambayo imetoka kupoteza mchezo wake wa mwisho kwa mabao 3-0 dhidi ya Kenya baada ya kushinda miwili ya mwanzo kwa kuichapa Djibouti 13-0 na Ethiopia 1-0, na kushika nafasi ya pili katika Kundi B, ambalo Wakenya waliibuka vinara.

Kuelekea mchezo huo wa leo, tayari Kocha wa Kilimanjaro Queens, Bakari Shime ameeleza makosa madogo madogo ambayo ameyabaini katika mechi zilizopita ameshayafanyia kazi na kilichobaki ni vijana wake kutekeleza kile alichowaelekeza kukifanya dimbani leo.

Aidha, kuongezeka kwa ari na morali ya ushindi kama ambavyo Shime alilieleza Nipashe juzi, kunaongeza matumaini zaidi kwa Watanzania kuona Kilimanjaro Queens ikishinda mchezo wa leo na kutinga fainali kabla ya kuubeba kabisa ubingwa huo kwa mara ya tatu mfululizo.

Tunaamini kwa kiwango kilichoonyeshwa na Kilimanjaro Queens katika michuano hiyo hadi kufikia sasa, itaendelea kutembeza vipigo hadi fainali na kilichobaki ni Watanzania kuendelea kuiombea ili iweze kuitoa nchi kimasomaso.

Lengo letu ni kutaka kuona kombe hilo linabaki nchini na Kilimanjaro Queens ikiandika rekodi kwa kulibeba kwa mara ya tatu mfululizo bila kuruhusu nyavu zake kutobolewa msimu huu.

Lakini pia, Nipashe tunatamani kuona wachezaji wa Kilimanjaro Queens wakishirikiana kumlisha mipira winga mshambuliaji, Donisia Minja, anayeshika nafasi ya pili kwa upachikaji mabao kwenye michuano hiyo, ili aweze kuibuka na Kiatu cha Dhahabu kwa kuwa mfungaji bora.

Hadi sasa Donisia anashika nafasi ya pili katika orodha ya wafungaji akiwa na mabao matano sawa na Nalukenge Juliet wa Uganda, wakiwa bao moja nyuma ya kinara Jentrix Shikangwa wa Kenya.

Hivyo, tunatamani kuona juhudi za dhati za ushindi kwa wachezaji wa Kilimanjaro Queens zikienda sambamba na kutoa pasi nyingi za mwisho kwa Donisia ili wakitetea ubingwa huo uende sambamba na Kiatu cha Dhahabu kubaki hapa nchini.

Hivyo, ili Kilimanjaro Queens na Donisia waweze kutekeleza hayo, ni wazi pamoja na kuiombea, lakini mchezaji wa 12 uwanjani ambaye ni mashabiki, ni muhimu sana katika kuwapa sapoti kwa kuwashangilia mwanzo mwisho.

Katika hilo, tunatamani kuona mashabiki na Watanzania kwa ujumla wakibadilika na kujenga utamaduni wa kushangilia mwanzo mwisho hata kama Kilimanjaro Queens itatangulia kufungwa.

Tunatambua Uganda itaingia uwanjani ikiwa na lengo la kupata bao la mapema ili kuweza kuunyamazisha uwanja, lakini hata kama ikitokea hivyo mashabiki hawana budi kuendelea kuishangilia Kilimanjaro Queens mwanzo mwisho ili kuwaongezea morali ya kufanya vizuri katika mchezo huo. Tunaitakia kila la kheri Kilimanjaro Queens.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Bahati ina miujiza, lakini haina ahadi

Na Barnabas Maro

**KW**A kawaida bahati huweza kuleta mambo ya ajabu, lakini haitabiriki. Kwa hiyo ni vigumu kuitabiri bahati. Methali hii yatuhimiza tufanye bidii bila kutegemea miujiza.

Timu mbili zinapopambana, kila moja huwa na lengo la ushindi, hasa moja inapocheza nyumbani. Timu ya nyumbani inaposhindwa na timu ngeni, washangiliaji wenyeji hunyamazishwa kabisa na wageni!

Husemwa "Bahati ni chudi" yaani bidii au jitihadi/tijihada. Methali hii yatufunza umuhimu wa kuwa na bidii katika mambo tufanyayo.

Kila timu inayoingia uwanjani kushindana na nyingine huwa na lengo la ushindi. Nathubutu kusema hata wendawazimu hawawezi kucheza ili washindwe! Ushindi ni hali ya mtu/watu kufanikiwa katika jambo alilokuwa/walilokuwa akiliwania/wakiliwania.

Wahenga walisema: "Mcheza kwao hutuzwa" wakiwa na maana kuwa mtu anayecheza kwao hupewa zawadi au kutunzwa vizuri. Methali hii hutumiwa kutufunza kwamba mtu anayelifanya jambo fulani vizuri au inavyopasa, hutuzwa au hupewa zawadi.

Mechi yetu ya kandanda dhidi ya Libya iliyochezwa Tunisia kisha Taifa Stars kupoteza kwa kufungwa 2-1 imekuwa na maneno mengi ya lawama dhidi ya wachezaji, hasa kapteni wao, Mbwana Samatta na kocha wao, Mrundi Etienne Ndayiragije.

Kwa waliofuatilia mchezo ule kwa makini watakubaliana nami kuwa Libya ilibebwa na mwamuzi (refa) wa mchezo ule kwa kuizawadia timu hiyo penalti ya bure.

Naandika hivyo kwa sababu chanzo cha penalti iliyopewa Libya na mwamuzi kutoka Malawi haikuwa halali kwani mpira uligonga ugoko/muundi (mfupa wa mguu kuanzia kifundo hadi kwenye goti) wa beki Bakari Mwamnyeto wa Taifa Stars na si mkono kama alivyoamua mwamuzi!

Tukio lile lilioneshwa kwa kurudiwa mara kadhaa (-a kiasi maalum) ili kuthibitisha mpira haukugusa mkono wa mlinzi wa Taifa Stars ila uligusa ugoko wake tu.

Kinachonishangaza ni kwa nini viongozi wa TFF waliofuatana na Taifa Stars hawakulalamikia dhuluma (kitendo cha kumnyima mtu haki au stahiki yake; uonevu) ile; au hawakuona?

Kama hawakuona, walisinzia? Kama ndivyo, walikwenda Tunisia kufanya nini? Au walikubaliana na uamuzi wa refa Mmalawi aliyechezesha mechi ile?

Kadhia hiyo inaiweka Taifa Stars katika hali ngumu kwani itabidi ishinde michezo iliyosalia bila kupoteza hata mmoja. Mechi hizo ni kati yake na Tunisia jijini Tunis na kurudiana nayo jijini Dar es Salaam.

Je, haiwezekani penalti ile ni sababu kubwa iliyowakatisha tamaa wachezaji wa Stars kipindi cha pili hata kufungwa bao la pili lililoipa 'ushindi' wa chee (rahisi) timu ya Libya? Jambo lingine linalonikera ni upangaji wa michezo ya Ligi Kuu inayoendelea humu nchini. Kwa nini TFF inashindwa kabisa kupanga ligi ili timu zote zicheze mechi bila kutofautiana kwa idadi kubwa ya michezo?

Nilihesabu mechi za ligi za wenzetu zilizochezwa na timu za Ulaya msimu huu wa ligi yao mpaka Novemba 20, 2019 na kupata matokeo yafuatayo:

England: Mpaka tarehe niliyoitaja, timu 20 za ligi hiyo zilikuwa zimecheza mechi 12 kila moja. Hispania: Timu zote 20 zilikuwa zimecheza michezo 13 isipokuwa mbili tu ndizo zilizocheza michezo 12. Ujerumani: Timu zote 18 zilikuwa zimecheza mechi 11 kila moja wakati timu 20 za Italia zikiwa zimecheza mechi 12 isipokuwa timu mbili ndizo zilizocheza mechi 11. Ufaransa nayo ina timu 20. Katika hizo, timu 18 zimecheza mechi 18 ilhali timu mbili tu ndizo zilizocheza mechi pungufu, yaani 12 kila moja.

Tarehe hiyo hiyo niliyoandika makala unayosoma sasa, ligi ya Tanzania yenye timu 20 zikuwa zimecheza kama ifuatavyo:

Yanga mechi 5, Azam FC mechi 7, Simba FC, Polisi Tanzania na Ndanda FC mechi 9 kila moja. Kagera Sugar, Lipuli FC, Tanzania Prisons, Namungo FC, JK Tanzania, Alliance FC, Coastal Union na Biashara United zikiwa zimecheza mechi 10 kila moja,

Timu zilizocheza mechi 11 kila moja ni Mtibwa Sugar, Ruvu Shooting, Mbao FC na Singida United inayozibeba timu 19. Haimaanishi kuwa timu za wenzetu hazina michezo mingine ya kimataifa, hasha! (sivyo kabisa.) Zinashiriki sana mechi za kimataifa ila zina mpangilio mzuri usiovuruga ligi zao.

Kinachowashinda viongozi wa TFF kuwa na mpangilio mzuri ili timu zetu kucheza mechi zisizotofautina kama wenzetu ni kitu gani?

Nadhani ni vema atumwe kiongozi mmoja ughaibuni akajifunze upangaji wa michezo ya Ligi Kuu kama inavyokuwa kwao. Najua kila mmoja atataka kwenda huko ili kufuta tongotongo.

# Mkufunzi jeshi asakwa tuhuma za mauaji

**Na Elisante John,** SINGIDA

JESHI la Polisi mkoani Singida linamsaka mkufunzi msaidizi wa Jeshi la Akiba, Said Ng'imba, namba MG 129191, kwa tuhuma za mauaji ya vijana wawili waliokuwa kwenye mafunzo ya Jeshi la Mgambo Kata ya Mudida wilayani Singida.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Sweetbert Njewike, alisema wanafunzi hao wanadaiwa kufariki dunia baada ya kupewa adhabu iliyopitiliza, kwa kutakiwa watumbukie ndani ya dimbwi lililojaa maji ya mvua.

Alidai vijana hao walipoteza maisha kutokana na kushindwa kumudu kuogelea.

Alidai mkufunzi huyo aliwapa adhabu hiyo baada ya kutuhumiwa kutoshiriki ipasavyo mafunzo ya Novemba 19, mwaka huu.

Aliwataja wanafunzi hao wa mafunzo ya awali Jeshi la Mgambo kuwa ni Ismail Hussein (22), mkazi wa Kijiji cha Sefunga na Emmanuel Hamisi (20), mkazi wa kijiji cha Mudida wilayani Singida.

Kwa mujibu wa Kamanda Njewike, vifo hivyo vilitokea Jumatano katika Kijiji na Kata ya Mudida, Tarafa ya Mtinko wilayani humo, yalikokuwa yanafanyika mafunzo hayo.

Alisema muda mfupi baada ya kutokea kwa vifo hivyo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, walipata taarifa kutoka kwa raia wema na kufika haraka kwenye eneo la tukio na kufanikiwa kuopoa miili hiyo.

"Vijana hao baada ya kutumbukia ndani ya dimbwi, hawakuweza kuibuka, hali iliyosababisha mkufunzi huyo kutoweka haraka eneo la tukio na kukimbilia kusikojulika mpaka sasa, tayari juhudi za kumsaka zimeanza na tunaomba ushirikiano kwa wananchi," alisema.

Njewike alitumia fursa hiyo kuwaagiza wakufunzi wengine wote mkoani Singida, kuzingatia weledi katika kutoa mafunzo ili kuepusha vifo visivyokuwa vya lazima.

## Mradi wa uzalishaji maziwa wazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA kwa kushirikiana na taasisi ya kimataifa ya uwezeshaji mifugo ya maziwa ya Land O'lakes, imezindua mradi wa miaka mitano wa uzalishaji bora wa maziwa na kuongeza soko la bidhaa za maziwa nchini ifikapo mwaka 2024.

Akizindua mradi huo jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema mradi huo unazingatia uwezeshaji kwa maofisa ugani mikoa 26 ya Tanzania Bara na kwamba utaanza kutekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro.

Prof. Elisante Ole Gabriel alisema mradi huo utazingatia kuwezesha maofisa ugani, pembejeo na uzalishaji wenye tija hadi kufikia mahitaji ya soko la bidhaa za maziwa ndani na nje ya nchi.

Alisema mradi huo ambao unaungwa mkono na nchi kadhaa na wahisani ikiwamo Marekani, unalenga pia kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli katika kuhakikisha nchi inakuwa katika uchumi wa viwanda na kujitegemea kiuchumi.

Katibu Mkuu alisema kwa sasa Tanzania bado ina uzalishaji mdogo wa maziwa licha ya kuwa na idadi kubwa ya mifugo, huku wafugaji na sekta ya kilimo ikikabiliwa na changamoto za ugani na kwamba mradi huo unakuja na ufumbuzi wa kuhakikisha uzalishaji maziwa unaongezeka maradufu.

Aliwataka Watanzania kupokea mradi huo kwa mikono miwili na kuondokana na ufugaji wa kuchunga na kujikita zaidi kwenye ufugaji wa kibiashara na kuiwezesha nchi kuongezea thamani bidhaa za maziwa kwa mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

Pia alisema alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka huu, Tanzania ina ng'ombe milioni 30, mbuzi milioni 20.5, kondoo milioni 5.5, lakini wanaotumika katika uzalishaji maziwa ni milioni mbili tu.

Mratibu wa mradi huo nchini Tanzania kutoka Land O'lakes, Neema Mrema, alisema mradi pia unatekelezwa katika nchi kadhaa barani Afrika na umeonyesha mafanikio makubwa kwa kuinua pato la wafugaji na nchi husika kwa ujumla.



Mbunge wa Jimbo la Solwa, Ahmed Salum, akisikiliza kero za wananchi wa Kijiji cha Ngokolo, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga juzi, na kuzitatua, sambamba na kunadi wagombea wa serikali za mitaa kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM). **PICHA: MARCO MADUHU**

## JPM aonya utapeli wa madai ya fidia

**INATOKA UK. 2**

wamebaki wachache, kuwa na makao makuu Dodoma msichukulie kama chanzo au fursa ya kutapeli serikali hilo halitawezekana serikali ina njia zake za kufanya kazi.

"Utapeli ni kosa la jinai, watu wadai maeneo wanayostahili ndio maana hapa nimewaletea viongozi ambao ni makini, watumieni hawa kutatua matatizo yenu," alisema.

Rais alitolea mfano kuwa kuna eneo jirani na Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), lilitengwa eneo la kuzika viongozi na alikataa kuzikwa Dodoma na kila mmoja alikataa kuzikwa huko, hivyo serikali ikarudisha eneo hilo kwa wananchi. "Nawaomba ndugu zangu wa Dodoma tunapopeleka madai kwa serikali tuyapime madai, wamejitokeza matapeli mnawachangia na fedha wanajifanya mimi ndio nitakuwa mwenyekiti wa kamati ya kudai wale ni matapeli wanakula fedha zenu.

"Hata Dar es Salaam walijitokeza wakati tunajenga barabara ya Ubungo hadi Kimara tumebomoa bila fidia wakajitokeza mahakamani tukashinda kesi. Mjiepushe na matapeli kujenga makao makuu na serikali kuhamia sio fursa ya watu kupata fedha bure bure, serikali haina fedha za bure bure," alisisitiza.

Alifafanua kuwa anafahamu kukiwa na mikutano yake watu wanajitokeza wanalia.

"Mtu anatoka nyumbani halii akifika hapa analia lia, kwanini usitoke nyumbani unalia hadi hapa, wala siwasikilizi, sidanganywi wala sidanganyiki, we utalia hapa ukienda nyumbani utanyamaza lazima Dodoma tuijenge hatuwezi kuchelewa kuijenga Dodoma kwa mikwamo ya ovyo, tumekuja kuibadilisha Dodoma.

"Kuna miradi mingi imejengwa Dodoma mambo ni mengi, lazima Dodoma ijengwe nawaambia wana Dodoma siku moja mtakumbuka, kuhamia Dodoma kulikuwa kumeshindikana Nyerere kazungumza tangu mwaka 1973 mimi nilikuwa darasa la sita, miaka 40 imepita, kuamua kuhamia hapa kunahitaji moyo wa kigogo," alisema.

Aliwataka kutokwamisha mafanikio yaliyopatikana kwa kuwa watu watawashangaa, makao makuu yangeweza kupelekwa hata mkoa wa Singida kwa kuwa ndio katikati ya nchi.

Hata hivyo, alisema wale wenye madai ya halali yashughulikiwe wasidhulumiwe.

Kuhusu mkandarasi anayetekeleza mradi wa ujenzi wa soko na kituo cha mabasi, alimtaka kukamilisha kwa muda uliopangwa.

Kadhalika, alisema katika kituo hicho cha mabasi kuna eneo la wamachinga, hawatatozwa fedha yoyote bali watatumia vitambulisho vya ujasiriamali walivyopewa.

"Hawa wenye vitambulisho hakuna kuwadai hela, bahati nzuri tutakuwa tunabanana hapa hapa, nitakuwa nikipita pita," alisema.

Alisema miradi yote ikikamilika Dodoma itakuwa ya kisasa.

"Tutaunganisha kituo cha mabasi na stesheni ili mtu akishuka apitilize moja kwa moja hadi ndani ya stendi, na pia tutaunganisha na uwanja wa ndege utakaojengwa wa Msalato, lakini tutaunganisha na mji wa serikali, ili kurahisisha usafiri," alisema.

Hata hivyo, aliwatoa hofu wakazi wa Dodoma kuhusu changamoto ya maji na kudai kuwa ipo mbioni kutekeleza mradi wa ujenzi wa bwawa la Farkwa ambalo litahudumia watu wa Jiji la Dodoma na maeneo jirani.

## RC Tabora ageukia malezi ya mimba

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

WANAUME kuwekeza katika ujauzito wa wake zao kunasaidia kupata watoto wenye uchangamfu na makuzi mazuri na hivyo kuwa na taifa bora la baadaye.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, wakati akifungua mkutano wa siku moja wa kukuza uelewa kuhusu malezi na makuzi ya watoto.

Alisema kwa mujibu wa wataalamu, malezi na makuzi mazuri ya watoto yanaanzia siku mama anapopata ujauzito na kuendelea.

Mwanri alisema hatua hiyo itawezesha mtoto kuwa mchangamfu kuanza akiwa tumboni na hata baada ya kuzaliwa.

"Mzazi anapaswa kuongea na mtoto wake maneno mazuri tangu akiwa tumboni na baada ya kuzaliwa kuwa naye karibu kwa kumfundisha mambo mbalimbali kwa ajili ya kumkuza katika malezi bora," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, aliitaka jamii kuepuka kutoa lugha za matusi na zisizofaa kwa watoto, akieleza kuwa zinawasababisha kujenga roho ya ukatili.

"Utakuta mzazi atamtukana mtoto wake matusi mazito kama vile kichwa kama tofali...mbwa...mpumbavu ..mjinga... maneno kama hayo hayamjengi mtoto, bali yanamfanya kuwa mkatili siku za usoni.

"Tujifunze kuwaambia watoto maneno mazuri ambayo yatawakuza katika maadili mema na kuwafanya kuwa raia wema," alishauri.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Honaratha Rutatinisibwa, alisema ubongo wa mtoto unakuwa tayari kupokea mambo mbalimbali yatakayokea katika maisha yake tangu siku ya kwanza anapozaliwa.

Alisema ni vema wazazi kujenga tabia ya kuongea na watoto wakiwa angali tumboni mwa mama zao na baada ya kuzaliwa ili kuwajengea uchangamfu na makuzi mema.

Mganga huyo alisema anatambua wazazi wengi kubanwa na majukumu, lakini ni vema wakatenga muda wa kucheza na watoto wao ili kuwaongezea uchangamfu.

# Magufuli ashusha neema Polisi

**INATOKA UK. 3**

vyombo vingine vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa mnayofanya ya kuhakikisha nchi inakuwa salama, serikali siku zote itasimama kwenye upande wenu kuhakikisha hii amani inapatikana kila siku," alisema.

Hata hivyo, alisema anatambua bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na makazi ya askari.

"Serikali inatambua na kadri uwezo wa serikali unavyoimarika tutaendelea kushughulikia suala la makazi na changamoto nyingine, nyinyi Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama, wito wangu mwendelee kufanya kazi kwa bidii kwa uadilifu na uzalendo," alisema.

Aliwaasa kuendelea kufanya kazi kwa kuwa taifa linawategemea kwani bila wao hakuna kitakachofanyika, huku akiwaonya makamanda wa juu kutowanyanyasa makamanda wa chini na wa chini wasiwanyanyase wa juu.

Alitoa wito kwa watu wanaojenga mradi huo kuhakikisha zinakamilika kwa wakati.

Awali, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, alisema katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Magufuli kiasi cha Sh. bilioni 35.7 kimetolewa kwa ajili ya vyombo vya ulinzi na usalama vilivyopo wizara hiyo na kiasi cha Sh. bilioni 188 kwa ajili ya kulipa madeni ya askari na wazabuni.

Akitoa taarifa ya hali ya uhalifu, Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP) Simon Sirro, alisema kwa sasa makosa makubwa ya jinai yamepungua kwa asilimia 24.9 ikiwa ni matunda ya mchango wa miaka minne ya uongozi wa Rais Magufuli.

Aidha, alisema makosa kama ya unyang'anyi wa kutumia nguvu yamepungua kwa asilimia 54.2 wakati makosa ya barabarani kwa asilimia 69.4.

Kuhusu uchaguzi, IGP alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa amani na utulivu kwa kuimarisha ulinzi na usalama kila kona.

"Pia lile suala lililotokea Mtwara tayari baadhi ya watu wameanza kukamatwa na tumejipanga vizuri, hatutamvumilia mtu atakayefanya mambo ya ovyo," alisema.

# MOI sasa yajivunia matibabu ya kibingwa

**INATOKA UK. 3**

kuwahudumia au vifaa vilikuwa havitoshi," alisema.

Alisema baada ya kuona hali hiyo Rais Magufuli aliagiza MOI ipewe kiasi cha Sh. bilioni 16.5 ili kukamilisha mradi wa jengo jipya na kununua vifaa tiba.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, MOI imenunua vifaa vya kisasa vya CT Scan, MRI, X-Ray zikiwamo zinazohamishika, Ultrasound, Fluoroscopy na vya vifaa vya kisasa vya maabara, chumba cha uangalizi maalum (ICU) na cha upasuaji.

"Vifaa hivi ni vya kisasa na ni sawa na vile vinavyotumika kwenye hospitali za kimataifa na kwa hospitali za India tayari tumeshawazidi. Pia tuna vyumba tunavyoweza kumlaza kwa matibabu mtu wenye hadhi yoyote," alisema.

Dk. Boniface alifafanua kuwa kati ya wagonjwa waliohudumiwa katika miaka hiyo minne ni pamoja na waliofanyiwa upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu (Athroscopy) wagonjwa 870.

Wengine walifanyiwa upasuaji wa ubongo 880, watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi 2070, upasuaji mkubwa wa mfupa wa nyonga wagonjwa 618 na waliobadilishiwa nyonga ni 900.

Alisema MOI ni kituo cha mafunzo ya udaktari na kwamba ndani ya miaka hiyo minne, imezalisha madaktari bingwa 50 wa upasuaji wa mifupa, ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu, idadi ambayo haijawahi kufikiwa.




Ofisa Mawasiliano na Ushawishi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo (WiLDAF), Neema Meremo (kushoto), akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu uzinduzi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia unaotarajiwa kufanyika mkoani Dodoma Jumatatu. Kulia ni Nancy Mpiri wa WiLDAF na Pastory Buberwa wa Shirika la Mkuki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Asimulia alivyotaka kuwakimbia mapacha wanne

**INATOKA UK. 3**

"Ni kitu ambacho kilinishtua mno na ilibaki kidogo tu nizimie kwa kweli kwa nilivyowaona wale watoto niliporudi wodini sikuwa natamani kuwaona tena," alisema.

"Hapo ndipo niligundua kwa nini wanawake wanakimbia watoto wao kwa sababu wanapokimbia unaweza kuwalaumu bure kumbe siyo wao kuna vitu vigeni vinakuwa vimeingia ndani ya vichwa vyao," alisema.

Baada ya siku tatu, alisema watoto wawili walizidiwa na mmoja moyo ulikuwa umesimama wakati mwenzake tangu alipozaliwa alikuwa hawezi kupumua vizuri.

"Hili ndilo tatizo linalowapata watoto njiti, mapafu yao yanakuwa hayajakomaa kama watoto wengine. Wawili waliendelea kukaa Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) na wenzao wodi ya kawaida za watoto," alisema.

Beatrice anasimulia kuwa wakati hali hiyo ikiendelea kwa watoto wake, alifuatwa na daktari na kuambiwa kwamba anatakiwa kukamua maziwa kwa ajili ya watoto.

"Nikiwa na msongo wa mawazo wa watoto wangu niliowaona, wengine wakiwa ICU naambiwa nikamue maziwa kila baada ya saa mbili au tatu, nilishindwa kufanya hivyo kutokana na hali niliyokuwa ninaipitia, nilitafutiwa mfadhili akaninunulia maziwa," alisema.

Kwa mujibu wa Mbawala, changamoto iliyopo ni kwamba kwa Tanzania bado hakuna benki ya maziwa ya watoto ambayo ni muhimu.

Alisema wakati wakihangaikia maziwa, daktari alimtaka awafanyie watoto hao malezi ya mtindo maarufu kama Kangaroo kwa kuwaweka kifuani kwake kwa ajili ya kupata joto lake kwa saa nane kila siku ili kusaidia ukuaji wao.

"Namshukuru Mungu nilikuwa na mwanaume ambaye tulisaidiana, ila hatukuweza kuwafanyia hivyo kwa saa nane kila siku ila tulikuwa tukifanya kwa saa moja au tatu kadri tunapopata muda," alisema.

Alisema alikaa hospitali miezi miwili na nusu na gharama kwa ujumla aliyotakiwa kuilipa ilikuwa ni zaidi ya Sh. milioni 100 ambayo ameshukuru Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa kumsaidia kulipa.

"Kwa vyovyote vile nisingeweza kulipa na matibabu ya watoto njiti kwa hospitali za binafsi au serikali ni gharama kubwa na wazazi wa kawaida ni ngumu kumudu, naiomba serikali ipitie hizi gharama na kuongeza vifaa vya kuwasaidia kupumua," alisema.

Alisema kwa sasa watoto wake wametimiza mwaka mmoja na miezi kumi na kati ya watoto hao wanne, mmoja wa kike alifariki dunia.

Daktari bingwa wa watoto wachanga hospitalini hapo, Yasser Abdallah alisema takwimu za Tanzania zinaonyesha kati ya watoto milioni 1.5 wanaozaliwa kwa mwaka, 255,000 ni njiti. "Kiwango cha vifo vya watoto wachanga kimefikia 21 kwa vizazi hai 1,000 ambapo ni takribani vifo 30,000 kwa mwaka. Matatizo ya uzazi njiti yanachangia kwa asilimia 24 ya vifo vyote vya watoto wachanga ambapo ni takribani vifo 7500 kwa mwaka.

Watoto njiti 20 hufa kila siku," alisema. Naye Mkuu wa Idara ya Watoto katika Hospitali ya Aga Khan, Mariam Noorani, alisema idadi kubwa ya watoto njiti wanaofanikiwa kuishi wanaendelea kuwa katika hatari ya matatizo ya muda mrefu kama kujifunza, ukiziwi na upofu.



Wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Idara ya Biashara, Monika Milinga (kulia) na Paulo Temu, wakichangia damu katika makao makuu ya jumuiya hiyo, jijini Arusha juzi, kama sehemu ya wiki ya maadhimisho ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwake, ambapo kilele chake kitakuwa mwishoni mwa mwezi huu. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Mtumishi Tanesco adaiwa kughushi, kudandia zabuni

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MFANYAKAZI wa Tanesco, Mkoa wa Arusha (jina linahifadhiwa) amelalamikiwa kughushi nyaraka na kufanya kazi za mkandarasi kinyume cha sheria za shirika hilo.

Akitoa malalamiko hayo jana jijini hapa, mbele ya waandishi wa habari, mkandarasi Simon Sulley, kutoka kampuni ya Elinc, inayofanya kazi Wilaya ya Loliondo alisema mfanyakazi huyo wa Tanesco alighushi nyaraka za kampuni yake na kuzitumia kufanya kazi zake, jambo alilosema ni kinyume cha sheria.

Alisema baada ya kugundua mfanyakazi huyo anafanya hivyo, alitoa taarifa ofisi ya Tanesco wilayani Longido, kwa Meneja wa Wilaya, na mshukiwa kuitwa , kuhojiwa na kukiri kutumia nyaraka za mkandarasi huyo.

Alitaja moja ya kazi zake alizofanya kuwa ni zabuni ya kufunga umeme ndani ya nyumba za watu iliyotangazwa na Tanesco.

Alieleza kuwa zabuni hiyo aliishindania na kushinda, lakini alishangaa kuona mfanyakazi wa Tanesco anafanya kazi hiyo ambayo yeye aliipata.

"Hapa nikalazimika kuanza kufuatilia, maana haiwezekani nishinde mimi halafu kazi afanye mwingine, nikaja kugundua huyu mfanyakazi anatumia nyaraka zangu kufanya kazi zangu," alisema Sulley.

Aidha, alieleza kuwa kwa mujibu wa Sheria za Shirika hilo na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati ya Maji (Ewura), mfanyakazi wa Tanesco harusiwi kufanya kazi za mkandarasi, lakini akaeleza kushangazwa na kitendo cha mfanyakazi huyu kuchukua nyaraka zake na kufanyakazi zabuni ambayo haimhusu.

"Huyu mtu baada ya kumbaini alikiri mbele ya Meneja wa Wilaya kuwa anatumia jina langu kufanya kazi ambayo mimi nimepewa na shirika na baada ya kukiri aliniomba kunilipa fedha zote alizozipata kwa kazi hiyo ambazo ni Sh. 9,000,000, lakini hadi sasa hajanipa na ananikwepa," alisema.

Sulley alieleza kuwa baada ya kuvuta subira kwa muda mrefu bila majibu alipeleka malalamiko yake ngazi ya mkoa za shirika hilo, ambao walimsikiliza na kumtuma Ofisa Ulinzi wa Tanesco ili kumuhoji.

"Lakini tangu hatua hiyo ifanyike hajajibiwa chochote na kinachonishangaza zaidi mtuhumiwa huyu amehamishwa kituo cha kazi, kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Longido na kupelekwa Tanesco Arusha," alisema.

Aidha, alisema mfanyakazi huyu ameiletea hasara kubwa kampuni yake na kuiomba serikali imsaidie alipwe hasara aliyoipata na kumchukulia hatua mfanyakazi huyu kwa kuvunja sheria.

Gazeti hili lilimtafuta mtuhumiwa bila mafanikio, hata hivyo, Nipashe iliwasiliana na Meneja wa Tanesco Mkoa wa Arusha, Herini Mhina na kukiri kupokea malalamiko hayo na kwamba tayari alishamtuma ofisa ulinzi wa shirika kufanya uchunguzi wa tuhuma hizo na bado anaendelea na mahojiano naye.

"Kama atakuwa na makosa lazima ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria, namwomba mlalamikaji avute subira na sisi tunalifanyia kazi. Siyo kwamba tumeliacha na sisi hatujamhamisha eneo la kazi. Bali aliomba uhamisho mwenyewe na hata siku moja hatuwezi kumhamisha mtu kwa vile anatuhumiwa," alisema Mhina.

Alisema sheria haimruhusu mfanyakazi wa Tanesco, kufanya kazi ya mkandarasi hivyo ikibainika malalamiko haya ni ya kweli hatua zitachukuliwa.

# Mkurugenzi OBC asota mahabusu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha, jana imeshindwa kuendelea na kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mkurugenzi wa Kampuni ya Otterlo Business Limited (OBC), kutokana na upelelezi wa kesi hiyo kutokamilika.

Akizungumza jana katika mahakama hiyo, mbele ya Hakimu Gwantwa Mwankuga, wakili wa serikali Ahmed Khatibu, alisema kesi hiyo imefikishwa mahakamani kutajwa ila kutokana na upelelezi kutokamilika aliomba tarehe nyingine ili itajwe tena.

Baada ya kuwasilisha ombi hilo, wakili wa utetezi Elvaison Maro, alisema hana pingamizi na hata kama wanahoja wanazihifadhi mpaka watakapoona inafaa kuzitoa.

Hakimu Gwantwa aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 4, mwaka huu itakapotaja tena.

Mollel anakabiliwa na makosa 10 likiwamo la kukwepa kodi na utakatishaji fedha haramu, unaodaiwa kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 12.4.

Mollel ni miongoni mwa watuhumiwa walioandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP),kuomba kukiri mashtaka yanayomkabili.

Awali Oktoba 18, mwaka huu, wakili Valentine Nyalu, aliomba ahirisho fupi la shauri hilo la uhujumu uchumi namba 22 la mwaka huu kwa madai kuwa wanategemea kufika mahakamani hapo na makubaliano na upande wa serikali.

Mollel bado anaendelea kusota katika Gereza Kuu Kisongo baada ya kukamatwa Februari mwaka huu kwa mashtaka hayo ambayo hayana dhamana.

# Mil. 57/- zatengewa vijana A/Mashariki

**Daniel Sabuni na Zanura Mollel,** ARUSHA

VIJANA wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wanatarajia kushindana kwenye shindano la kutangaza kazi na mafanikio ya EAC, linalolenga kuongeza uelewa wa mtangamano huo.

Katika juhudi za kuwaunganisha vijana hao Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) litatumia Dola 25,000 (takribani Sh. milioni 57), kwa ajili ya shindano la wanafunzi 30 wa vyuo vikuu vya nchi wanachama.

Wahusika watakaoshindana kutengeneza video inayohusu mafanikio na shughuli za EAC.

Mkuu wa Mawasiliano wa Shirika la GIZ, Karari Duncan, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye makao makuu ya EAC, wakati wa mkutano na wanahabari pamoja na wanafunzi wa vyuo mbalimbali vya nchi wanachama waliofiki kuadhimisha kilele cha miaka 20 ya EAC.

Duncan alisema fedha hizo zimelengwa kuunganisha vijana wa nchi sita wanachama wa jumuiya, lakini pia kueneza uelewa wa shughuli na mafanikio yaliyofikiwa kwa miaka 20 tangu kuzaliwa kwa EAC, ili kuwa na nguvu moja kiuchumi na kupunguza umaskini kwa wananchi wake.

"Washindi 30 ambao watatengeneza video zitakazogusa vigezo watafaidika na fedha hizo, video inatakiwa iwe ya sekunde 30 hadi 45 kuonyesha EAC imefanya nini, hili litahusisha watu milioni 10 na video hizo moja ya kigezo ni kuziweka kwenye mitandao ya kijamii ambayo inafikiwa na watu wengi," alisema.

Alisema lengo la EAC na GIZ ni kuwaunganisha vijana ambao ni kundi kubwa zaidi lenye nguvu na chachu, ambao mbali na kufaidika na jumuiya hiyo, lakini ni wepesi kuelezea mafanikio na malengo kwa makundi mengine, ili kuunganisha nchi hizo. Kwa mujibu wa Karari, maadhimisho ya miaka 20 ya ERAC pia yamelenga kuhakikisha elimu inakuwa na ubora kwa nchi zote na ndiyo sababu ya kukutanisha wanafunzi, wataalamu ili kubadilishana uzoefu kwa lengo la kuboresha upande wenye udhaifu.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Balozi Liberat Mfumukeko, alisema, EAC imekuwa ikiweka mkazo kuwezesha viwanda vya nchi wanachama, ili kuwa na viwanda vingi vitakavyopunguza changamoto za ajira kwa vijana na wananchi wengine.

Pia alisema EAC imewezesha kujengwa kitengo cha moyo jijini Dar Es Salaam katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Matibabu ya Figo nchini Kenya, ili kupunguza safari za wagonjwa, waliokuwa wakitoka nje ya nchi zao kwenda ng'ambo kutafuta matibabu kwa gharama kubwa.

Alisema Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), imekuwa nguzo kwa maendeleo ya Jumuiya ya AFrika Mashariki kwa kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa miradi mingi.

# Mtaalamu akoshwa kilimo cha mpunga

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TANZANIA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha mchele mzuri, safi na ulio na thamani kubwa kulinganisha na nchi inazopakana nazo.

Sambamba na hilo, Tanzania pia imetajwa kuwa nchi yenye idadi kubwa ya wanawake wanaozalisha kwa wingi zao hilo, ikizalisha wastani wa tani tano hadi nane kwa hekta.

Hayo yalibainishwa na mtaalamu wa kilimo kutoka Jimbo la Zambezi, Msumbiji, Jaime Gado, alipotembelea nchini akiwa na timu ya wataalamu wa zao la mpunga.

Wataalamu hao, baadhi yao wakitokea Japan, wameingia nchini kwa ajili ya kubadilishana ujuzi na kujifunza kutoka kwa wakulima wa Tanzania kuhusu namna ya kuzalisha mpunga bora.

Gado alisema licha ya kuwa na mashine zilizochakaa na ubovu wa miundombinu, zikiwamo barabara, bado mkulima wa Tanzania amekuwa na ari ya kuzalisha mpunga ulio bora kulinganisha na nchi nyingine.

"Tumeona changamoto kadha wa kadha, lakini bado mkulima huyu amekuwa akizalisha kilicho bora, tatizo ni uhakika wa soko, naishauri mamlaka husika kuangalia namna ya kuwasaidia mkulima huyu ili auuze kwa wingi katika nchi za Bara la Afrika.

"Nipende pia kuwapongeza Jica (Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan) kwa kuweka utaratibu wa kuongeza thamani ya zao hili kwa kusaidia kusimamia makubaliano kati ya wanunuzi na wakulima wa Tanzania kupitia kwenye mradi wa Tanrice 2 kwani umekuwa mkombozi kwa wakulima wengi hususani waliopo kwenye skimu ya Lower Moshi," alisema.

Awali, akizungumza wakati wa mafunzo hayo ambayo yalilenga kubadilishana uzoefu na wataalamu wa kilimo nchini, Mshauri Mkuu wa Kiufundi katika Mradi wa Maendeleo ya Uzalishaji wa Mpunga wa Tanrice 2, Monitori Tomitaka, alisema idadi kubwa ya wazalishaji wa mpunga ni wanawake.

Alisema kwa mwaka 2014, Tanzania ilizalisha tani 925 kwa hekta na ina eneo kubwa linalolimwa mpunga, hivyo akashauri wakulima kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa ili kuongeza thamani ya mpunga wanaozalisha.

Mtaalamu kutoka nchini, Shedrack Msemo, alitaja vikwazo vya zao hilo kuwa ni pamoja na ubovu wa miundombinu ya kuingia kwenye mashamba ya wakulima, kutokuwa na mashine bora za ukoboaji wa mpunga na mashine za kuvunia mpunga.

# CCM wazidi kupeta uchaguzi wa mitaa

**Na Mary Mosha,** MWANGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro kimeendelea kujihakikishia ushindi katika uchaguzi wa serikali za mitaa baada ya mgombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji cha Raa wilayani Mwanga, Amiri Mfinanga (CUF) kujitoa kisha kujiunga na chama tawala hicho.

Amiri alitangaza azma ya kujiondoa katika kinyang'anyiro cha kugombea nafasi hiyo jana, katika mkutano wa kampeni wa kumnadi mgombea uenyekiti wa kijiji hicho kupitia CCM.

Mwanachama mpya huyo wa CCM alipokewa na mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho, Joseph Tadayo, aliyemkabidhi kadi ya uanachama. Akitangaza kuondoka katika Chama cha Wananchi (CUF),

Amiri alidai sababu za uamuzi wake huo ni pamoja na kutaka kuunga mkono jitihada za maendeleo zinazofanywa na Rais John Magufuli katika ujenzi wa taifa.

Alidai sababu nyingine ni uamuzi wa uongozi wa juu wa CUF kujiondoa katika uchaguzi wa serikali za mitaa huku wagombea wakiachwa pasi na kujua cha kufanya ilhali walikuwa wamejiandaa kwa uchaguzi.

Amiri alikabidhi barua yake ya kujivua kugombea nafasi hiyo kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Raa, Rita Tarimo, huku akishangiliwa na umati wa wanachama wa CCM, wakiwamo wagombea wa nafasi za uenyekiti wa kitongoji na vijiji vya tarafa ya Usangi wilayani Mwanga.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake (UWT) Mkoa wa Kilimanjaro, Zuhura Chikira, alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kuwachagua wagombea wa CCM ili washirikiane na viongozi wa kitaifa kuwaletea maendeleo katika sekta mbalimbali. Uchaguzi huo umepangwa kufanyika kesho ukitarajiwa kuhusisha wapigakura zaidi ya milioni 19. Tayari vyama kadhaa vya upinzani, kikiwamo chama kikuu cha upinzani, Chadema, vimetangaza kujitoa katika uchaguzi huo kwa madai mchakato wake umetawaliwa na uonevu dhidi ya vyama vya upinzani.



Mwezeshaji wa mafunzo ya ujenzi wa nguvu ya pamoja katika kupambana na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, Asseny Muro, akiwaeleza kwa mukhtasari wanaharakati 30 kutoka wilaya sita za mkoa wa Kilimanjaro jana, juu ya vuguvugu la ukombozi wa mwanamke kimapinduzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Tume yaanza kupima mionzi katika kahawa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

TUME ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) imeanza kupima mionzi kwenye mazao ya kibiashara yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi, ikiwamo kahawa, ili kulinda afya za walaji na soko la bidhaa zinazotoka nchini.

Mkuu wa Idara ya Huduma za Ufundi na Kinga ya Mionzi, Denis Mwalongo, aliyasema haya jana mjini Moshi alipozungumza na wanunuzi wa kahawa kutoka ndani na nje ya nchi.


Alisema tume hiyo imelazimika kuanza upimaji huo baada ya kubaini wakulima wanatumia kemikali kwenye mazao ya kahawa wakati wa uzalishaji, hali ambayo inasababisha soko la kahawa kushuka kutokana na wanunuzi kutaka kahawa ya kilimo hai kisichotumia kemikali za viwandani.

"Utafiti unaonyesha kuwa, wakulima wengi hutumia kemikali nyingi wakati wa uzalishaji wa kahawa, hali ambayo inasababisha kukwamishwa kushuka bei kwenye soko la dunia. Serikali haikubaliana na hali hii na ilishaanza kuweka mikakati ya kufanya zao hili kuwa na bei itakayokuza uchumi wa nchi," alisema.

Msafirishaji wa kahawa kwenda nje ya nchi, Geofrey Charles, alisema bei ya kahawa itokanayo na kilimo hai ni nzuri kulinganishwa na kahawa inayozalishwa kwa kemikali.

"Kwenye soko la dunia, kahawa ya kilimo hai ina bei nzuri sana, ni wajibu wa serikali kupitia halmashauri zake kuhakikisha inawahimiza wakulima kujikita katika kilimo hai ili kuleta tija kwenye zao la kimkakati la taifa," alishauri.

Blass Eligy, mkulima wa kahawa, akizungunzia vikwazo vya zao hilo, alisema wakulima wanakumbana na matatizo ya kutokuwa na pembejeo au kuziwa pembejeo hizo kwa bei ghali huku bei ya kahawa ikiwa chini.





Kamishna wa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi nchini Kenya, Rose Macharia, akizungumza na wanachama wa klabu ya maadili ya Shule ya Sekondari Dodoma juzi, kwa lengo la kujifunza namna ya uendeshaji wa klabu zinazosimamiwa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ripoti za utafiti ziwe na lugha inayoeleweka

**Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeziagiza taasisi zinazofanya utafiti katika maeneo mbalimbali kuwasilisha matokeo yake kwa lugha nyepesi kwa walengwa ili iwe rahisi kuelewa madhara na faida za kazi walizotafiti.

Hayo yalibainishwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru, akizungumza katika kongamano la nne la kitaaluma la kuwasilisha matokeo ya utafiti wa mchango wa ukuaji wa viwanda na biashara katika maendeleo ya uchumi wa nchi.

Ndunguru alisema umuhimu wa utafiti ni lazima mlengwa afikiwe kwa sababu ndiye mtumiaji na anapaswa kujua matokeo ya kile anachokifanya kama kinamletea faida au hasara.

"Naomba niwapongeze Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa kuwasilisha matokeo ya utafiti mbalimbali mliofanya tena kwa lugha nyepesi. Hii itasaidia walengwa kujua nini kinaendelea katika kilimo au biashara wanazofanya," alisema Ndunguru.

Kutokana na hilo alisema taasisi nyingine au vyuo vinavyofanya utafiti zihakikishe zinawasilisha kwa lugha nyepesi kwa walengwa jambo ambalo litafanya jamii kupata matokeo chanya ya tafiti zinazofanywa na taasisi au vyuo hapa nchini.

Alisema ikifanywa hivyo kadri siku zinavyokwenda umuhimu wa tafiti mbalimbali zinazofanya utasaidia kuleta matokeo chanya.

Akizungumzia upande wa chuo hiko alikipongeza kutokana na kupanda kitaaluma kila siku hali inayoonyesha jitihada zinazofanya na uongozi wake.

"Hata hivyo mnapaswa kuendelea kuongeza bidii ili siku moja CBE iwe namba za juu katika vyuo vya elimu ya juu," alisema.

Mbali na hilo Naibu Katibu ambaye alimwakilisha Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha katika kongamano hilo aliwataka CBE kuendelea kuelimisha na kutoa mafunzo sahihi kwa jamii juu ya elimu ya biashara, ikiwamo kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaaluma kwa wananchi.

Lengo la kufanya hivyo ni kusaidia jamii kufanya biashara yoyote ile kwa weledi mkubwa na kuleta matokeo chanya.

Mkuu wa CBE, Profesa Emanuel Mjema, aliishukuru serikali kutokana na jitihada zinazofanywa kuhakikisha chuo hiko kinatoa elimu bora kwa jamii ambayo inasaidia watu kujua kanuni za biashara ambazo wanakwenda kufanya.

Profesa Mjema alisema kupitia jitihada zinazofanywa na serikali chuo hicho kitaendelea kuwa bora kitaaluma na kuongeza uchumi wa viwanda kupitia wanataaluma wanaohitimu ambao watakwenda kuwa walimu kwa jamii zinazowazunguka.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo, George Shumbush, alisema serikali ikiwekeza itakuwa imesaidia kuongeza mwongozo mzuri katika ngazi mbalimbali ndani ya chuo hiko.

# IOM kufanya kazi zaidi na Tanzania

**Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wahamiaji (IOM) limesaini mkataba wa miaka miwili na Tanzania kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa maofisa uhamiaji ili kuwa na uelewa wa kutosha wa jinsi ya kudhibiti wahamiaji haramu.

Akizungumza wakati wa kusaini mkataba huo juzi jijini Dodoma Mwakilishi Mkazi wa IOM, Dk. Qasim Sufi, alisema shirika hilo limeamua kusaini mkataba na Tanzania baada ya kupata manufaa mazuri kupitia mkataba wa miaka mitano uliomalizika.

Alisema mafunzo hayo yanatolewa katika Chuo cha Uhamiaji cha Kanda kilichopo Moshi mkoani Kilimanjaro kinachotoa taaluma ya uhamiaji kwa maofisa uhamiaji wa Tanzania na nje ya nchi.

Dk. Sufi alisema mkataba wa awali Tanzanzia iliutekeleza vyema kwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa maofisa wa uhamiaji na hivyo kukabiliana na wahamiaji haramu katika nchi yake.

"Kutokana na makubaliano yaliyomalizika tumeamua kusaini tena mkataba na Tanzania kwa lengo la kuendelea kutoa elimu hiyo, na mkataba huu unakuja baada ya chuo hicho kuonekana kimefanya vizuri awali, lakini lengo la hayo yote ni kupunguza wahamiaji haramu," alisema Dk. Sufi.

Hata hivyo, alisema kuwa suala la kupambana na wahamiaji haramu si la nchi moja bali ni la kila nchi barani Afrika ikiwa na lengo kuhakikisha unaungana na shirika hilo ili kukabiliana na changamoto hiyo.

Kwa upande wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, alisema IOM watapeleka maofisa kutoka nchi mbalimbali kwa ajili ya kuwa na mafunzo ya mara kwa mara katika kupambana na wahamiaji haramu.

Waziri Lugola alisema katika kuhakikisha nchi inaendelea kuwa salama serikali imekubaliana na shirika hilo kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kupata mafunzo, teknolojia na baadhi ya vifaa katika kukabiliana na wahamiaji haramu.

"Mkataba huu unalenga kutusaidia katika vifaa, teknolojia pamoja na mafunzo, hasa kipindi hiki ambacho kunakuwa na wahamiaji haramu wengi kukimbilia Tanzania, lakini idara zinazohusika zimekuwa zikifanya jitihada kukabiliania na changamoto hiyo, hivyo niendelee kuwataka Watanzania kutoa ushirikiano pindi wanapoona watu wanaowatilia shaka," alisema Kangi.

Alisema kati ya vyombo vya ulinzi na usalama ni vema maofisa wa vyombo hivyo kuwa na taaluma hiyo ya teknolojia ya utumiaji vifaa vya kudhibiti wahamiaji haramu.

Alisema mkataba huo ambao unalenga kusifia vifaa na mafunzo ni muhimu sana na umeonyesha Chuo cha Uhamiaji kufanya vizuri ndio maana wamerudia kusaini kwa mara nyingine mkataba huo.

Mbali na hilo alitoa wito kwa Watanzania ambao wanatabia ya kuwahifadhi wahamiaji haramu kuacha tabia hiyo kwa sababu serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani maofisa uhamiaji wako makini kutokana na mafunzo waliopata watawabaini.

Kamishna wa Uhamiaji, Maurice Kitinusa ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda, alisema tukio la kusaini mkataba huo ni muhimu sana kwa sababu Luna faida kubwa mbili.

Alisema moja ya faida hizo ni kwamba wamewawezesha chuo kujiendesha wenyewe kupitia mafunzo wanayopata pamoja na vifaa wanavyotoa kwa chuo.

# Awataka wafanyabiashara kujifunza elimu ya biashara

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAFANYABIASHARA na wazalishaji nchini wametakiwa kujifunza elimu ya biashara ili bidhaa zao ziweze kuingia katika soko la ushindani nje na ndani ya nchi.

Mhadhiri wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Dodoma, Dk. Nasibu Mramba, ambaye ni meneja wa masuala ya elimu, utafiti na ushauri wa kitaalamu, alisema.

Mramba alisema moja ya changamoto kubwa inayochangia kuzorota kwa bidhaa za wafanyabiashara ni kukosekana kwa elimu ya biashara kwa wanajamii.

"Elimu ya biashara kwa wafanya biashara na wazalishaji muhimu sana hivyo ni lazima kitu kifanyike ili watu wapate elimu hiyo na kuingia katika soko la ushindani," alisema Dk. Mramba.

Alisema elimu zaidi inatakiwa ili kutatua changamoto za biashara na wazalishaji ambayo itawawezesha kutengeneza bidhaa bora ambazo zitaingia katika soko la ushindani la kimataifa.

"Ukosefu wa elimu kwa wafanyabiashara ni tatizo kubwa linapaswa kuangaliwa na kufanyiwa kazi," alisema Dk. Mramba.

Akizungumzia kuhusiana na kongamano hilo alisema lina umuhimu kwa jamii kwa sababu kwanza linatumia Kiswahili ambacho kinamwezesha mkulima na mfugaji kupata ujumbe halisi kiufasaha.

Alisema lugha nyepesi humfanya mlengwa hadi wa vijiji kuelewa na kujua tatizo linalomkwamisha kusonga mbele.

Alisema katika kongamano hilo mada za utafiti 26, zinazowasilishwa zina manufaa makubwa kwa jamii kutokana kwamba waliohudhuria kongamano hilo ni wakulima, wafugaji na wafanyabiashara wa ngazi ya chini hadi juu.

Alisema watu hao watafaidika ikiwamo kujua nini kinachowakwamisha katika biashara au kilimo wanachofanya.

Kutokana na hilo alisema CBE itaendelea kuandaa makongamano hayo kila mwaka kwa lengo la kuwainua wafanyabiashara na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali.





Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma (kulia), akitoa taarifa kwa waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, kuhusu mitihani ya taifa ya darasa la nne, sita na kidato cha pili, ambayo inatarajiwa kuanza wiki ijayo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanafunzi darasa la nne, sita kuanza mitihani wiki ijayo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATAHINIWA 87,945 wa darasa la nne na la sita kutoka shule za serikali na za binafsi wanatarajia kuanza mitihani yao Jumatatu ijayo.

Kati ya hao 55,635 ni wa darasa la nne na 32,310 wanasoma darasa la sita, ambao watafanya mitihani wiki ijayo yao ya taifa kuanzia Jumatatu ijayo.

Aidha, watahiniwa 34,469 wanatarajiwa kufanya mitihani ya kuingia kidato cha tatu itakayofanyika siku ya Krismasi Desemba 25, mwaka huu.

Akizungumza na wanahabari Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, alisema kuwa kati ya watahiniwa hao wa kidato cha pili wanawake ni 18,502 na wanaume ni 15,967 sawa na upungufu asilimia moja ikilinganishwa na idadi ya watahiniwa waliofanya mitihani hiyo mwaka jana.

Waziri huyo aliwataka wazazi na walezi kuwa karibu zaidi na watoto wao wanaofanya mitihani hiyo ili kuhakikisha wanafika katika vituo vyao vya mitihani kwa wakati na kuweza kutumuia haki yao ya elimu.

"Wizara inawaomba madereva na makondakta wa magari ya abiria kuwa na busara na hekima kwa wanafunzi wakati wa kwenda shuleni na kurudi ili wawahi kufanya mitihani yao vizuri."

Alieleza kuwa ufanyaji wa mitihani unahitaji amani na utulivu hivyo amezinasihi jamii asiyehusika asijaribu kusogea kituo cha mitihani kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria na kanuni za mitihani.

Waziri huyo aliwataka watahiniwa wote kujiepusha na vitendo vinavyokwenda kinyume na kanuni za mitihani ikiwamo kufanya udanganyifu.

"Atakayebainika kwenda kinyume na taratibu za mitihani hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufutwa kwa matokeo yake," alisema.

Hata hivyo, Waziri alisema kuwa jumla ya watumishi sita wa wizara hiyo wamesimamishwa kazi kutokana na kuhusika na udanganyifu wa mitihani ya taifa ya kidato cha pili mwaka 2018.

Alieleza, kuwa wakati watumishi hao wakiwa wamesimamishwa kazi taratibu nyingine za kisheria zinaendelea na zitakapokamilika watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani.

# Oman, Zanzibar kuwa na mshikamano zaidi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imeeleza kufurahishwa na juhudi za kiongozi Mkuu wa Oman, Sultan Qaboos Bin Said, katika kukuza maendeleo ya Zanzibar na kuendeleza udugu wa watu wa nchi mbili hizo.

Akizungumza wakati wa hafla ya maadhimisho ya miaka 49 ya Taifa la Oman iliyofanyika Mjini Zanzibar, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mohammed Aboud Mohammed, alisema hatua hiyo ni kielelezo cha uhusiano wa kidugu kati ya serikali na watu wa nchi hizo.

Aliwaambia washiriki kuwa watu wa Oman chini ya Sultan Qaboos, wamekuwa mstari wa mbele kuimarisha ushirikiano huo wa miaka mingi na kuhakikisha Zanzibar inapata maendeleo katika kila nyanja, ikijitolea kwa dhati kutoa misaada mbalimbali ya kiuchumi, kidiplomasia na utamaduni.

"Katika ushirikiano huo serikali zetu zote mbili, Zanzibar na Tanzania, zimeweka upendeleo maalum wa kuthamini ushirikiano huo, viongozi wetu wakuu Sultan Qaboos, Rais John Magufuli na Ali Mohamed Shein, wamekuwa mfano wa kuendeleza na kuimarisha udugu wetu," alieleza.

Alitaja baadhi ya misaada ambayo Oman imetoa kwa Zanzibar, kuwa ni kugharamia matengenezo makubwa ya jumba la kihistoria Beit El Ajaib, ambayo mkataba wake umetiwa saini hivi karibuni na tayari maandalizi yameanza.

Waziri Aboud pia alisema, viongozi hao wameanzisha ushirikiano kusaidia katika nyanja tafauti za kihistoria kwa kuendeleza majengo ya kale, wakilenga kuweka mazingira mazuri ili historia isitoweke.

Aidha, alisema utaratibu uliowekwa wa ziara za viongozi baina ya nchi hizo, ni sehemu ya mipango ya kuimarisha uhusiano wao kwa manufaa ya wananchi wa Oman na Zanzibar.

Kwa upande mwingine, alipongeza ubalozi mdogo kwa juhudi zinazochukuliwa kuhakikisha uhusiano huo unakuwa madhubuti na wa kudumu, akitoa nafasi kwa kila jambo linaloonekana litaleta faida kwa Zanzibar.

Balozi Mdogo wa Oman, Dk. Ahmed Hamood Al Habsi, alisema Serikali chini ya Sultan Qaboos, Oman imeshuhudia maendeleo makubwa ambayo yamebadilisha maisha ya wananchi wake na kuyafanya bora kuliko miaka ya awali.

Aidha, alisema nchi yake imejizatiti kuisaidia Zanzibar katika sekta mbalimbali zikiwamo za kiuchumi, na kuwafungulia milango Wazanzibari kutumia fursa za uhusiano wa kihistoria katika kukuza udugu na mwingiliano wa kibiashara na kijamii.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, Waziri wa Vijana, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Balozi Ali Abeid Karume, alisema kuna kila sababu ya kuendeleza uhusiano uliopo kati ya Oman na Zanzibar ambao ni wa kidamu.

# Shein aahidi kufanya kweli kisiwa cha Uzing'bwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BAADA ya kilio cha muda mrefu cha wananchi wa kisiwa cha Uzing'bwa kuhusu ubovu wa barabara, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohammed Shein, amewahakikishia kuwajengea barabara wakati wowote kuanzia sasa.

Aidha, amewataka kuamini kuwa anatekeleza ahadi aliyotoa ya kujenga barabara na daraja la kisasa na kwamba serikali imo katika upembuzi yakinifu na imeshamkabidhi kazi hiyo mjenzi mwelekezi kufanya michoro ya njia hiyo pamoja na daraja kwa awamu ya kwanza tayari imeshafanyika na hivi sasa iko katika awamu ya pili.

Rais Shein ambaye Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, aliyasema hayo wakati akifungua jengo jipya la tawi la chama katika kisiwa hicho kilichopo mkoa wa Kusini Unguja.

"Bado ahadi niliyoitoa ya ujenzi wa barabara na daraja la kisasa la kuelekea kisiwa cha Uzi iko pale pale," alisema Dk. Shein.

"Serikali ya awamu ya saba ninayoiongoza mimi nitaanza na ujezi huo wa barabara na kama haikumaliza basi awamu ya nane italikamilisha," alisema Dk. Shein.

Aidha, alieleza kwamba juhudi za makusudi zinafanywa na serikali katika kuhakikisha mradi huo unafanikishwa haraka iwezekanavyo na kwa umuhimu wake huenda likapangiwa fedha katika bajeti ijayo ili lianze kufanyiwa kazi.

Alieleza kuwa panapofunguliwa tawi la CCM ni vyema kuwakumbusha umuhimu wa wazee kwani ndio hazina kubwa ya chama hicho.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar alieleza kuwa chama hicho kimeagiza kwamba matawi yake yanayojengwa yaendane na sifa ya chama hicho.

Alieleza kuwa matawi mengi ya CCM yamefungulíwa, lakini hilo liko kipekee na lina historia muhimu kisiasa hasa kuanzia zama za chama cha ASP pamoja na CCM.

Akisoma taarifa juu ya ujenzi wa ofisi ya tawi la CCM Ng'ambwa, Sharifa Maabadi Othman, kwa niaba ya Katibu wa Tawi, alisema kuwa lilianzishwa mwaka 1957 chini ya ASP na mwenyekiti wa kwanza, Juma Hamadi Simai (marehemu).

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI NOVEMBA 23, 2019



**BURNA BOY AYAPONZA MATAMASHA 'SAUZI'** Soma UK.20



## NAJIONA KIPEPEO

# Vanessa amkubali Rotimi kuliko Jux

BASI SAWA




## ‘Wajukuu wa Magu’ wamsifu babu yao

WATOTO Mnora Abdallah na Nasra Abdallah, wametoa ngoma yao ya kwanza ambayo ni maalum kwa Rais John Magufuli.

Wasanii hao ambao ndio kwanza wanachipukia katika muziki wameachia wimbo huo ‘Babu Magu’ mwanzoni mwa wiki hii.

Ndani ya wimbo huo kuna mashairi ambayo yanamsifu kazi nzuri ya Rais na juhudi anazofanya katika kuhakikisha Watanzania wanaishi maisha bora.



## Msondo kusindikiza uzinduzi wa albamu ya Talent Band


BENDI Kongwe ya Msondo Ngoma, ni kati ya makundi yatakayoshiriki katika tukio la onyesho la kutambulisha albamu ya saba ya Talent Band ya jijini Dar es Salaam.

Onyesho hilo limepangwa kufanyika Ijumaa ya Novemba 29 katika ukumbi wa Kisuma, uliopo Temeke, jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia na mwandishi wa habari hizi, Hussein Jumbe, alisema, albamu yao hiyo inajulikana kwa jina la ‘Subiri Nifikie’ ambayo ni ya saba tangu kuanzishwa kwa bendi hiyo miaka kumi iliyopita.

Alisema, sambamba na kutambulisha albamu hiyo, pia onyesho litakuwa maalum kwa ajili ya kuzindua studio mpya ya kundi hili la Talend Band iliyopo eneo la Tua Ngoma, jijini Dar es Salaam.

“Ni onyesho ambalo litakuwa ni la aina yake kwa sababu litakuwa na matukio makubwa matatu ambayo yote yanaihusu Talent Band kama familia moja.”




# NAJIONA KIPEPE
# Vanessa amkubali Rotimi

MWANAMUZIKI nyota, Vanessa Mdee, amesema mpenzi wake Rotimi, anampatia amani ya moyo na kujiona yupo kama kipepeo kwenye maua.

Akizungumzia uhusiano wake kupitia Ayo Tv, Vanessa amesema mwanaume huyo amembadilisha maisha yake baada ya kuacha maisha ya kujificha na yasiyo na uhalisia.

Amesema tangu wajenge uhusiano wa kimapenzi na Rotimi, amejikuta akiwa na mapenzi mazito na kwamba ndiye atakuwa mume wake.

“Ni mwanaume mwenye hekima, anapenda watu na huwezi kumdanganya kutokana na maisha yake kuwa halisi sana,” amesema Vanessa.


Rotimi ambaye amezidiwa na Vanessa miezi mitatu ya kuzaliwa, ameelezewa kupenda kumwo mrembo huyo pamoja na kum kuwa na muda wa kupumzika ya kazi.

Amesema walikutana baada masha moja la Marekani, na w bulishwa na rafiki yao na hap hisia za mapenzi zilipoanza k

“Kila nikizungumza naye na nina furaha najiona kama kipe

## INSTA-TWITTER





**Kuna** muda macho ya watu yanaongea ukweli zaidi kuliko midomo yao - **Dulla Makabila.**



**Hahaha** eti ‘Jua linawaka hatari halafu serikali ipo kimya tu’-Wananchi tuna nongwa, hadi jua tusaidiwe? Khaa!! - **Juma Lokole.**



## ...O ... kuliko Jux

...ngoza ...shauri ... baada

... ya ta- ...walitam- ...o ndipo ...ati yao. ...jisikia ...epeo.

Sikupata mtu wa kuniambia pumzika, kwa mara ya kwanza yeye aliniambia natakiwa niwe na muda wa kutulia nafanya kazi sana kama roboti," ameongeza kusema.

Hata hivyo, akimzungumzia mpenzi wake wa zamani Juma Jux amesema anamtakia kila la heri na Mungu ataendelea kumwongoza katika kazi zake.

## UNASEMAAA...

# 'SWAHILI FASHION WEEK' Jukwaa la mavazi linalosisimua

MSIMU wa mitindo umewadia ndani ya wiki moja katika Jiji la Dar es Salaam ambapo litapata joto baada ya pazia la Swahili Fashion kufunguliwa rasmi Desemba 6 mwaka huu.

Jumla ya wabunifu 34 watakonga nyoyo za wavaaji kwa kuonyesha mitindo mbalimbali ya mavazi ambayo vijana na wazee wanapagawa nayo.

Wabunifu watakaoshiriki ni kutoka Marekani, Afrika Kusini, Burundi, Uganda, Italia na Tanzania wanatarajia kushiriki maonyesho ya mavazi ya Swahili.

Akizungumzia maonyesho hayo, Mwasisi na Mwanzilishi wa Swahili Fashion Week, Mustafa Hassanali, amesema bidhaa za ubunifu wa mavazi kutoka Tanzania na Afrika kwa ujumla wataweza kubadilishana mawazo na wenzao wa nje.

"Wakati wote tumekuwa tukitilia mkazo thamani ya bidhaa za ubunifu za Afrika kwa kuhamasisha wananchi kununua bidhaa zilizotengenezwa Tanzania na Afrika," anasema.

Anasema pamoja na maonyesho ya mavazi ya jukwaani, pia kutakuwapo na maonyesho ya picha nyumbani kwa Balozi wa Italia, ambapo wabunifu wa mavazi hapa nchini wataweza kuonyesha na kuuza bidhaa zao mbalimbali ili kujiongezea kipato na kutafuta masoko.

Pia mwaka huu wataongeza kipengele kipya kwenye tuzo zao za Mbunifu wa Mwaka mikoani ambapo wataangalia waishio na kufanya kazi zao mikoa mingine tofauti na Dar es Salaam ili kuwapa nguvu ya kufanya kazi.

Vile vile mbunifu wa mavazi kutoka Italia Marta Zampoline atashiriki katika maonyesho hayo ili kubadilishana mawazo na wenzake kwa lengo la kujua changamoto zinazowakabili.

"Kama msemo wa Kiafrika usemavyo, ukitaka kufika mbali zaidi ambatana na wenzako siyo kusafiri peke yako," anasema.

Hassanali amewaomba Watanzania kununua bidhaa ambazo zimebuniwa na Watanzania ili kukuza uchumi wa nchi na maisha ya watu waliojikita katika sekta hiyo.

Ameongeza "Tuzo za Swahili Fashion Week zinaletwa kwa Watanzania na Green Telecom na kusimamiwa na Nexia SJ." Alisema.

Mbali na hilo pia watasherehekea na kutambua mchango wa wadau mbalimbali kwenye tasnia ya ubunifu ambapo tuzo kutoka vipengele 26 zitatolewa.

Anasema lengo la kuendeleza tasnia ya ubunifu Afrika bado linabaki mstari wa mbele kwa kupitia jukwaa hilo. Kwa upande wake, Rais wa Shirikisho la Sanaa za Ufundi Tanzania (TAFCA), Adrian Nyangemalle, amesema Tanzania inaelekea kwenye uchumi wa kati na watu wengi bado hawajafahamu maana yake.

"Hivi sasa wabunifu wa mavazi wanatakiwa wawe na ubunifu hasa kwenye umaliziaji wa nguo vinginevyo soko litachukuliwa na watu wengine," amesema.


Amesema wakishindwa kuwa na vitu vyenye ubora, Watanzania hata wateja wengine hawataweza kununua wataendelea kuchangamkia bidhaa za nchi zingine.

Amesema Swahili Fashion Week ni jukwaa kubwa la mavazi ambalo linachangia kukuza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Afrika.




## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Nchi** yetu imejaaliwa vitu vingi sana ila upendo ndio kila kitu **-Maua Sama.**



**Ukiyatizama** maisha kitaani ni kawaida kabisa, vijiweni, boda boda, daladala, mavazi ya kawaida, lugha Kiswahili. Lakini ukiyatizama kwenye mitandao ya kijamii huko maisha ni mazuri, lugha nyingi Kingereza, sasa mwamuzi ni wewe unajipima na uhalisia ulionao **- Nikki wa Pilli.**



**Wakati** mwingine tunashindwa kujua ni mtu yupi anafaa kuachwa na yupi anafaa kuvumiliwa. Na hapo ndipo tunajikuta kuvumilia wasiofaa na kuwaacha wanaofaa kuvumiliwa **-Johari.**

Kuumbe!



WASANII BONGO MPO!

# Wenzenu wanang'ara Grammy, nyie chuki, fitina

SAUTI ya filimbi imelia kwa wasanii wa Bongo, kwamba wakati umefika sasa kuanza kuitangaza nchi kwa kufanya kazi zenye ubora na zinazokubalika kimataifa.

Wakati wa kupigana vijembe na kuwekeana vikwazo katika kazi zao umekwisha, kwani Watanzania wanataka kuwaona nguvu na juhudi zao zinaelekezwa katika ubunifu na ufanyaji kazi kwa weledi.

Tanzania imebarikiwa kuwa na wasanii wazuri, lakini hawafanyi vizuri kutokana na kujengwa katika tabia za uchoyo, kutopendana na kuoneana wivu.

Hata hivyo kuchaguliwa kwa wasanii kutoka nchi nyingine za Kiafrika katika tuzo za Grammy inaleta funzo kwa wasanii wa Bongo kuachana na vurugu zao ili wajizatiti kufanya kazi nzuri zitakazowapaisha kimataifa.

Katika nchi ya Nigeria, wasanii wameacha mambo yote yatakayo warudisha nyuma, badala yake wanafanya kazi nzuri ambazo zimewatambulisha kimataifa na kutajwa katika tuzo nyingi maarufu.

Hivi karibuni Wanigeria walipagawa kwa furaha baada ya mwanamuziki kutoka nchini humo, Burna Boy kutajwa katika tuzo ya Grammy ya mwaka 2020.

Katika tuzo hiyo pia ametajwa mchekeshaji Trevor Noah kutoka Afrika Kusini kuiwania.

Burna Boy yeye ametajwa kwenye kipengele cha 'Best World Music Album" kupitia album yake ya African Giant.

Naye mchekeshaji, Trevor Noah yeye ametajwa kwenye kipengele cha 'Best Comedy Album' kupitia kazi yake ya 'Son of Patricia'.

Tuzo hizo kubwa kabisa duniani, zimepangwa kutolewa Januari 26, 2020, ambayo sherehe zake zitaongozwa na Alicia Keys.




JAYDEE

# Mama wa 5 Bongo fleva

Na Adam Fungamwango

MWANZONI mwa mwaka 2000 ndipo kulitokea mapinduzi makubwa ya muziki wa kizazi kipya nchini.

Muziki aina ya hip hop ulianza nchini mwishoni mwa miaka ya '90 na ilionekana kuwa ya kihuni na hata wazazi waliwakataza watoto zao kushiriki.

Kwa kiasi kikubwa wasanii Joseph Haule 'Profesa Jay' na Joseph Mbilinyi 'Sugu' ambao wote sasa ni wabunge na wenzao wachache, ndiyo walioirekebisha hip hop na kuimba maisha halisi ya kijamii, kuonya na kuelimisha, kitu ambacho kililegeza masharti ya wazazi wengi, ambao mbali na wao kuanza kupenda muziki huo kutokana na maudhui, hata baadhi wakaruhusu vijana wao kufanya muziki huo.

Kulegezwa kwa masharti ya wazazi yaliwaingiza kwenye gemu hata wasanii wa kike kwenye muziki huo.

Hapo pia kukatokea mageuzi ndani ya mageuzi, kwani baadhi wakaachana na muziki wa aina hiyo na kubuni staili nyingine ya muziki kama vile R&B.

Ni aina ya kuimba zaidi kuliko kutamka maneno, maarufu kama kufokafoka ambao ndiyo msingi wa muziki wa hip hop.

Hapo wakazaliwa wasanii wengi waliokuwa wanaimba na si wanaume tu bali hata wanawake.

Leo tunawaangalia wasanii wa kike wa mwanzo kabisa ambao waliingia kwa staili ya kuimba na kuwaacha kina Zay B na Sister P wakiendelea kufokafoka.

Hawa ndiyo taa au wafungua njia ya wasanii wengi wa kike tunaowaona leo kama kina Nandy, Maua Sama, Vanessa Mdee, Ruby na wengineo.

**1. STARA THOMAS**

Ni mmoja wa wasanii wa mwanzo kabisa wa kike mwa miaka ya 2000 kuingia kwenye Bongo Fleva na pia kwenye staili ya kuimba zouk, R&B na mitindo mingine inayoruhusu msanii kuimba zaidi kuliko kufoka.

Stara alipachikwa jina la 'Mama Tanzania'. Ni kwa sababu ya uimbaji wake ukishabihiana na Miriam Makeba ambaye aliitwa 'Mama Afrika'.

Hakupata tabu sana kuvuma kutokana na sauti yake ya staili yake ya kuimba kama Miriam.

Ngoma zilizompatia umaarufu ni 'Mimi na Wewe', 'Riziki' ambayo alishirikishwa na K Bazil, 'Nipigie', 'Nashindwa' na nyingine nyingi.

**2. HAFSA KAZINJA**

Katikati mwa miaka ya 2000, aliibuka mwanamama mmoja Hafsa Kazinja ambaye alitingisha kweli kweli na kutishia wanawake wenzake.

Cha ajabu ni kwamba alidumu kwa muda mfupi tu akatoweka. Ameibuka kwenye miaka ya hivi karibuni na kuwaambia mashabiki wake kwamba ameokoka na anamwimbia bwana, huku akiwa na nyimbo zake mbalimbali za Injili.

Kilichomfanya Kazinja kuwa maarufu na kujulikana kila kona ya nchi, akifungua milango au kuwashawishi akinadada wengine kuingia kwenye muziki huo ni ngoma zake mbili zilizobamba kweli kweli ambazo ni 'Mashallah', 'Nuru' aliyeshirikishwa na Ali Kiba na 'Pressure' aliyoshirikishwa na Banana Zorro.

**3. RAY C**

Huyu ni msanii wa kike aliyekuwa na mvuto zaidi kuliko wengine wote kati ya wale wanawake wa mwanzo kwenye muziki wa bongo fleva.

Jina lake kamili ni Rehema Chalamila, na jina la Ray C ni kifupi cha jina lake halisi.

Mbali na mvuto, alikuwa na uwezo mkubwa wa kuimba pamoja na kucheza kiasi cha kupachikwa jina la 'Kiuno hakina mfupa'. Naye anaingizwa kwenye orodha ya wasanii wa mwanzo wa kike waliofanya wazazi wawaruhusu mabinti zao kuingia kwenye muziki.

Pamoja na matatizo aliyoyapata hivi karibuni, lakini haiondoi ukweli kuwa ni mmoja wa wasanii bora wa mwanzo wa kike nchini.Sikiliza ngoma kama 'Mahaba ya Dhati', 'Umenimaliza', 'Uko Wapi', 'Sikuhitaji Tena', Sogea Sogea' na nyingine nyingi.

**4. MWASITI**

Mwasiti ni mmoja wa wasanii ambaye alipata umaarufu zaidi kutokana na sauti yake tamu kama asali.

Sauti nyororo na uwezo mkubwa wa kuitawala, ulimfanya kuwa maarufu sana na kuwa mmoja wa wasanii wa kike wa mwanzo walioliteka soko la muziki Tanzania.

Aliingia na ngoma moja iliyotetemesha watu 'Nalivua Pendo'. Baadaye alitoa ngoma nyingine iitwayo 'Siyo Kisa Pombe'. Mpaka sasa anaendelea na muziki.

**5. LADY JAYDEE**

Kwa sasa anamiliki bendi ya muziki wa dansi ambayo pia inapiga mchanganyiko wa nyimbo za aina nyingine. Kifupi ni muumini wa muziki halisi, ambao unapigwa kwa kutumia ala.

Lady Jaydee ni nembo wa muziki wa bongo fleva kwa wanawake. Ameshapiga muziki na wanamuziki wakubwa kabisa Afrika akiwamo marehemu Oliver Mtukudzi.Lakini ngoma zilizowafanya mashabiki washtuke na kujua kuna dada ameingia kwenye muziki wa bongo fleva ni 'Usiusemee Moyo'.

# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA




1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.**

PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0785652621**




## Samantha: Mkuki kwa nguruwe

**Na Adam Fungamwango**

KUNA msemo wa Kiswahili usemao, 'mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu', ukiwa na maana kwamba binadamu hupenda kumfanyia mwenzake mabaya, lakini akifanyiwa yeye hulalamika.

Ufafanuzi wa msemo huu ni kwamba mara nyingi kuna watu wana tabia ya kuwafanyia mabaya wenzao na kuchukulia poa tu, ila anapofanyiwa yeye, au ubaya kumrudia analalamika na kuona kwamba ameonewa, bila kukumbuka kuwa yeye ndiye aliyeanza.

Aliyetunga filamu ya 'Samantha', ameamua kufikisha ujumbe huu kwa jamii ili iweze kujifunza kitu kupitia sanaa hii.

Waliocheza filamu hii ni Isaa Mussa 'Claud', Selemani Barafu, Bi Hindu, Esha Buheti, Mariam Ismail 'Samantha', Mohamed Msisili na wengineo.

Samantha ni msichana anaishi kwenye familia ya kimaskini. Wazazi wake wanafanya kazi kwenye nyumba ya tajiri mmoja anayeitwa Claud.

Hata hivyo, familia ya tajiri huyo ina manyanyaso na inayojivuna. Msisili anamwita binti yake Samantha na kumwagiza akamwite mama yake kwa sababu hajisikii vizuri.

Anakwenda kumwita mama yake, lakini anakuta akifokewa na kupigwa na Bi. Hindu na binti yake Esha.

Hili linamuumiza roho binti huyo, lakini hana la kufanya. Anachofanya ni kumwambia tu, baba anamwita.

Haraka Samantha anarejea kwenye nyumba ya baba yake na kumkuta amekwishafariki. Anarejea tena kwa mama yake, lakini njiani anakuta amegongwa na gari katika harakati za kutaka kuvuka barabara ili aende kumwangalia mumewe.

Baada ya kufiwa na wazazi wake wote wawili, Samantha anabaki na masikitiko, lakini anaahidi kulipiza kisasi.

Kutokana na urembo wake, anamshawishi Claud na kuingia naye kwenye uhusiano wa kimapenzi na hatimaye ndoa.

Kisasi kinaanza. Siku isiyo na jina, wakati Claud yuko ofisini anapokea simu kutoka kwa mkewe Samantha kuwa ameingiliwa na majambazi nyumbani na kuua baba, mama na dada yake, huku yeye mkewe akiwa hospitalini baada ya kujeruhiwa. Haikuwa hivyo. Mauaji hayo ni mpango ulioratibiwa na mkewe Claud, Samantha kwa ajili ya kisasi cha wazazi wake.

Siku zikapita. Siku moja Claud akiwa ametoka matembezini alikutana na gari ambalo lilikuwa na mtu ndani na kuambiwa kuwa kuna msichana anataka amsalimie.

Aliposhuka kwenye gari yake na kwenda anamuone huyo mrembo ni nani alijikuta amepigwa na kitu kizito kichwani.

Akazindukia hospitalini. Dokta akamwambia ili apone ni lazima asafirishwe kwenda nchini India.

Anamwagiza mkewe anachuku pesa benki ili itapatikane nauli za kusafiri pamoja na matibabu.

Akiwa hospitalini hapo na rafiki yake Barafu anapigia simu na mkewe Samantha. Anamwambia ukweli wote. Kuwa alikubali kuolewa na yeye ili alipize kisasi cha vifo vya wazazi wake vilivyotokana na manyanyaso ya familia yake. Akamwambia kuwa yote yaliyotokea kuanzia vifo vya wazazi na dada yake, kupigwa na kitu kizito na hata daktari kuandika apelekwe India ilikuwa ni mkono wake.

Akamwambia ameshalipiza kisasi na tayari ameshachukua pesa benki na ametokomea kusikojulikana. Na hayo ni malipo kwa yale yaliyofanyika miaka ya nyuma.



## 'LIKES' ZIMEWAPONZA

# Mastaa wapigwa butwaa kuondolewa

WASANII maarufu nchini Marekani wametaharuki baaada ya kupata taarifa kwamba mtandao wa Instagram umeanza rasmi kuondoa 'Likes' kwenye posti za watumiaji wake.

Taarifa hiyo ambayo imetolewa mwanzoni mwa wiki hii imezusha hofu kwa mastaa hao na kuibua maoni tofauti kuhusu hatua hiyo.

Kazi ya kuondoa 'Likes' itahusu nchini Marekani pekee katika mabadiliko yanayofanyika kuboresha huduma ya mtandao huo pendwa.

Baada ya tangazo hilo kutoka, mwanamitindo Kim Kardashian, alijitokeza haraka na kupongeza hatua hiyo akisema ni nzuri kwani itapunguza chuki baina ya watumiaji na itaimarisha mahusiano yao.

Kauli ya Kardashian inatokana na baadhi ya wasanii kuwekeana chuki kutokana na wingi au uchache wa mashabiki wanaopendezwa na picha au ujumbe alioweka kwenye akaunti yake.

Hata hivyo, rapa mwenye utata Nicki Minaj, alipinga jambo hilo na kutishia kujitoa katika mtandao huo mara moja kama kazi hiyo itafanyika.

Akitumia akaunti yake ya Twitter amesema atajitoa kwa muda kwenye mtandao huo kwani hautamfanya ajisikie sawa kwa kuanza maisha mapya.

Instagram walitangaza ujio wa mabadiliko hayo Ijumaa iliyopita kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Adam Mosseri.

Marekani inakuwa ni nchi ya 8 kupata mabadiliko hayo, baada ya nchi za Australia, Ireland, Canada na nyinginezo kufanyiwa mabadiliko hayo.

# Burna Boy ayaponza matamasha Sauzi



MATAMASHA mawili yaliyopangwa kufanyika Afrika Kusini na kumshirikisha mwanamuziki nyota wa Nigeria Burna Boy yamefutwa kwa hofu ya kuzuka ghasia.

Boy alipangiwa kutumbuiza katika Tamasha la Afrika Ungana ( Africans Unite concerts ) katika miji ya Cape Town na Pretoria mwishoni mwa juma.

Tangazo kwamba angeonekana kwenye tamasha hili liliibua utata kwani mwezi Desemba wakati kulikuwa na wimbi la ghasia za ubaguzi nchini Afrika Kusini, Burna Boy aliapa kutokwenda tena nchini Afrika Kusini hadi serikali itakapotoa kauli.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter alisema; "binafsi alikuwa na uzoefu wa ubaguzi mikononi mwa Waafrika Kusini," mnamo mwaka 2017.



## Albam ya Rihanna hii hapa

MWANAMUZIKI staa wa Marekani, Rihanna, ametangaza kuachia album mpya itakayoingia sokoni mwezi Desemba 2019.

Mmoja wa wafanyakazi wa Kampuni ya Universal Music ametoa siri hiyo baada ya matayarisho ya kuisambaza album hiyo mpya kuwa katika hatua ya mwisho.

Awali Rihanna aliwahi kuzungumza juu ya ujio huo lakini hakuweka wazi kuwa ni mwezi gani itaachiwa.

## Kanye West ajiapiza kanisani

RAPA wa Marekani Kanye West ametinga katika kanisa la mchungaji Joel Osteen, na kujitangaza kwamba amemshinda shetani kwa kumwamini Mungu.

Kanye West aliweza kufika kwenye kanisa hilo na kuzungumza na watu wasiopungua elfu 16,000 huko nchini Marekani, na kueleza kwamba albamu yake mpya ni dalili njema ya kuwa karibu na Mungu.

"Nilikuwa na shetani kwa muda mrefu, leo nimeamua kumshinda na nyimbo zangu zimebadilika na kuwa za kumtukuza Mungu, inaweza kuzisikia katika albamu yangu mpya 'Yesu Ni Mfalme'.





## Offset ajiburudisha kutajwa Grammy

RAPA wa Marekani kutoka kundi la Migos, Offset amejifanyia jambo muhimu baada ya kutajwa kuwani tuzo ya Grammy ya mwaka 2019.

Offset ametajwa katika kipengele cha Best Rap Performance, na katika kushukuru kwake ameamua kujizawadi gari aina ya Ferrari yenye thamani ya Dolla laki 4 za Kimarekani

Kupitia ukurasa wa Instagram ameujulisha umma kuwa gari hilo litakuwa kumbukumbu kwake katika kuwania tuzo hiyo.

## Halima kwa urembo, si haba

MWIGIZAJI nyota wa Nigeria, Halima Abubakar, ametoa shukurani kwa mashabiki wake kwa kusaidia kupata tuzo ya staa anayependwa wa mwaka 2019.

Mrembo huyo alitajwa katika tuzo inayofahamika kama Nigerian Gold Face Awards, ambayo inalenga mwanamke mrembo anayekubalika na wengi.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, Halima alionyesha tuzo hiyo pamoja na kuwashukuru wote waliochangia yeye kushinda.



SAFU



MIONZI YA SHERIA

# Kiongozi S/Mitaa anahusikaje mikataba ununuzi wa ardhi?

Na John Juma
0716217615

SIKU za nyuma Nipashe iliwahi kuchapisha makala na kuandika namna au jinsi ambavyo sheria inakataza viongozi wa serikali za mitaa wakiwamo watendaji wa kata, wenyeviti wa mitaa, wajumbe kujipa jukumu la kuandaa na kusimamia mauzo na manunuzi ya nyumba au viwanja (ardhi).

Tena baada ya manunuzi hayo kuomba walipwe asilimia 10 ambazo hutolewa kwenye mazingira ambayo wanunuzi au wauza ardhi wanayafahamu.

Jambo hili ni kinyume cha sheria kwa kufanya hivyo viongozi na wahusika wanakosea na wanakiuka taratibu za kisheria.

Zaidi, hata asilimia 10 wanayowatoza kutokana shuruti hiyo ni kosa na ndiyo maana hauwezi kuona malipo yakifanyika aidha kwa kupitia, "akaunti maalumu ya serikali" au "mhusika au wahusika kupatiwa risiti za kielektroniki" ( EFD's) hivi tutakuwa tumekosea kusema huo ni wizi mtupu? Sitataka kutoa majibu lakini wananchi wanafahamu. Hivi baadhi ya viongozi hao, kutembea na mihuri ili kuidhinisha mauzo ya ardhi mitaani na wala si ofisini ni jambo jema? Ni utendaji wa kisheria? Kazi kwenu kutafakari.

ATHARI

Ni vizuri leo tukatazama athari zake, hususan baada ya kufanyika hivyo mhusika, je, ataruhusiwa kubadili jina katika hati ya ardhi kutoka kwa mmiliki wa awali kwenda au kuhamia katika jina lake, kama mmiliki halali anayefuatia baada ya huyo wa awali kumuuzia?

**NI MUHIMU**

Kufahamu kuwa athari yake huonekana zaidi kwa "ardhi iliyopimwa au zilizopimwa.

Aidha, Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999, kifungu cha 62(1) kinasema kuwa kila nyaraka (document) yoyote ya ardhi iliyosajiliwa ambayo itatumika katika mauzo, rehani, zawadi, kurithi au pango ni lazima iwe katika mfumo wa fomu maalum.

Halikadhalika, kifungu hicho kinaturejesha moja kwa moja katika Kanuni za Ardhi za mwaka 2001, inayosema ili kuziona fomu zinazohusika katika manunuzi ya ardhi na mahitaji yake.

Fomu ya kwanza ni "fomu namba 38" ambayo ni sawa na "mkataba wa mauzo" (contract for disposition). Fomu husika inalazimisha kuwa ni lazima iwe imegongwa muhuri wa wakili au kushuhudiwa na wakili.

Fomu ya pili ni "fomu namba 35" ambayo kisheria ni nyaraka ya "kuhamisha umiliki" (transfer of right of occupancy). Fomu hii nayo inatoa ulazima wa kushuhudiwa na kugongwa muhuri wa mawakili wa pande zote mbili, ambao ni wa upande wa mhamisha umiliki au muuzaji, na upande wa aliyepokea au mmiliki au mnunuzi.

Jambo au hatua hizi maana yake ni nini, endapo mhusika atapeleka au kuwasilisha nyaraka za ununuzi wa ardhi uliosimamiwa na kusainiwa ngazi ya serikali za mitaa bila ushuhuda wa wakili, kama sheria inavyoelekeza au kutaka, kwa lengo la kubadili jina hazitapokelewa na mamlaka husika? Kama vile Ofisi za Ardhi Wilaya kote au makao makuu ya Wizara ya Ardhi.

Isitoshe, kwa marejeo ya sheria (zote) hakuna sehemu yoyote ndani yake zimetaja au kutamka waziwazi kuzikabidhi serikali za mitaa jukumu hilo.

Kwa wachache waliowahi kufanya hivyo, na baadaye kutaka kuhamisha umiliki wanajua namna walivyogomewa kupatiwa ushirikiano.

Kimsingi, viongozi ngazi ya serikali za mitaa siyo kazi yao "kusaini" au "kugonga mhuri" katika nyaraka za kuuziana na kununua ardhi. Msaada wao unaishia kwa kusaidia utambuzi wa eneo na kwamba eneo husika halina mgogoro.

**MUHIMU**

Ieleweke vizuri kuwa wakili ndiyo mtu pekee anayetajwa na sheria hizo na hata kifungu cha 3 (1)(a) na (3), Sheria ya Wathibitisha Umma na Makamishna wa Viapo Sura Na. 12, kifungu cha 2, Sheria ya Mawakili sura Na. 341 zinathibitisha hivyo.

Sanjari na Sheria za Serikali za Mitaa Sura Na. 287 na 288, toleo la 2002 awali ikiitwa sheria Na. 7 na 8 za mwaka 1982.

Wakati huo huo kifungu cha 10 cha Sheria ya Mikataba sura Na. 345 kinatamatisha kwa kutilia mkazo kwamba makubaliano ya ardhi bila ya kuthibitishwa na wakili au mawakili wa pande zote mbili (2) ni batili." Hivyo, basi, kazi kubwa ya Serikali za Mitaa katika ununuzi wa ardhi ni "kumtambulisha muuzaji" ikiwa mnunuzi ataamua kwa hiari yake kuwatumia kutaka kumjua muuzaji hasa ni nani.

Au wakati mwingine mnunuzi atawahusisha ikiwa atahitaji kujua historia ya eneo lenyewe.

Kuwahusisha au kutowahusisha ni takwa la hiari, siyo takwa la kisheria au la lazima kwa tafsiri nyingine. Mnunuzi au muuzaji anaweza kuamua kuwahusisha au asiwahusishe viongozi hao.



KALAMU YA MWALIMU

# Watakaobahatika kesho tutumie kura zetu kuchagua viongozi

Na Reubeni Lumbagala

SAFU ya Kalamu ya Mwalimu imejikita katika kujadili masuala mbalimbali ya elimu na maendeleo ya jamii.

Kutokana na umuhimu wa uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika kesho, safu inatoa msisitizo kwa wananchi waliojiandikisha kwenda kupiga kura kwenye maeneo ambayo uchaguzi utafanyika na kwa yale ambayo wagombea wamepita bila kupingwa wasubiri maelekezo mengine.

Kabla ya vyama vya upinzani kujitoa kwenye uchaguzi huo, Jumapili Novemba 24, 2019 ndiyo ilikuwa siku ya kuwachagua viongozi hao kwa kuwapigia kura kazi ambayo ingeanza mapema asubuhi saa mbili hadi saa 10:00 jioni.

Kabla ya mambo kwenda ndivyo sivyo, ilitegemewa kuwa wananchi wenye umri wa zaidi ya miaka 18 waliojiandikisha na majina yao kuonekana katika vituo walivyojiandikishia, ndiyo ambao wangepiga kupiga kura kesho.

Mchakato wa uchaguzi huu ulianza Agosti, 2019, baada ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Selemani Jafo, ambaye ofisi yake husimamia uchaguzi huo, kutoa Tangazo la Uchaguzi kwa Umma.

Licha ya wapinzani kususia michakato mingi imefanyika hadi kufikia kesho siku ambayo kwa vyama vichache vinavyoshiriki, vikumbuke kuwa leo ndiyo mwisho kufanya kampeni kwa wagombea wa nafasi mbalimbali.

Nafasi zinazogombaniwa ni pamoja na wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za miji midogo, wa mitaa na wajumbe wa kamati ya mitaa hili ni kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake. Wengine ni wajumbe wa kamati ya mtaa . Katika upande huu kuna kundi la wanawake wote hao wanachaguliwa katika mamlaka za miji.

Nafasi nyingine ni wenyeviti wa vijiji, wajumbe wa halmashauri ya vijiji ambao ni kundi mchanganyiko wanaume na wanawake, pia wapo wajumbe wa halmashauri ya vijiji, wanawake na wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za wilaya.

Kesho kwa wanaoshiriki ni siku ya kuwachagua viongozi wa nafasi hizi za uongozi ili kuwapata wawakilishi bora kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Kama ambavyo baadhi ya wananchi walivyotumia muda wao kwenda kujiandikisha katika vituo mbalimbali ya uandikishaji wapiga kura, ndiyo ambavyo kama kusingetokea sintofahamu ya wapinzani kuususia ndivyo ambavyo Tanzania nzima wananchi wangepaswa kwenda kupiga kura kesho kuwachagua viongozi ambao watashirikiana nao katika kujiletea maendeleo.

> **Nafasi zinazogombaniwa ni pamoja na wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za miji midogo, wa mitaa na wajumbe wa kamati ya mitaa hili ni kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake. Wengine ni wajumbe wa kamati ya mtaa . Katika upande huu kuna kundi la wanawake wote hao wanachaguliwa katika mamlaka za miji.**

Hata hivyo katika sehemu ambazo uchaguzi unafanyika ni vyema kwenda kutimiza haki ya kidemokrasia.

Uchaguzi huo unatajwa katika Ibara ya 145 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kwa mujibu wa katiba unalenga kuimarisha demokrasia na kuleta maendeleo ya watu.

Licha ya vyama vya upinzani kujitoa itakumbukwa kuwa mara kadhaa walikuwa wanahimiza kuwa na utendaji kazi wa viongozi wanaowajibika. Lakini cha kushangaza wananchi pamoja na wakosoaji wa viongozi hawataki kushiriki uchaguzi wala kupiga kura. Ni vyema wananchi wakafahamu na kuzingatia kuwa njia pekee ya kupata viongozi bora ni kushiriki moja kwa moja katika kujiandikisha na hatimaye kupiga kura.

Pamoja na kwamba kumekuwa na kusuasua na upinzani kujiondoa uchaguzi huu wa serikali za mitaa, wananchi waendelee kujipanga na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ambao ni wa viongozi wakiwamo rais, wabunge na madiwani.

Tuseme kuwa hakuna sababu ya kuwalalamikia viongozi bila kupiga kura kwani haiwezi kusaidia kupata viongozi bora iwapo tutabaki nyumbani, badala ya kwenda kuwachagua viongozi kwa ajili ya maendeleo kwani viongozi bora ni chachu ya maendeleo.

Na wewe ndugu yangu kama mtaa, kijiji au kitongoji chako uchaguzi unafanyika nawe fanya vivyo hivyo, usibaki nyumbani, kapige kura kesho.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni: 0764 666349.**




Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza kwenye Tamasha la Kimataifa la Jinsia linaloandaliwa na TGNP kuhamasisha usawa wa kijinsia na ushiriki sawa wa wanawake na wanaume kwenye masuala ya maendeleo ya taifa. **PICHA: MTANDAO.**

# Kurunzi la kumulika uchaguzi kesho, 2020

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kesho ni siku ya uchaguzi wa serikali za mitaa licha ya kwamba unafanyika kwa baadhi ya maeneo, ni vyema kukumbuka kuwa umebakia mwaka mmoja kabla ya kufikia uchaguzi mkuu wa 2020.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), wanamtandao wa wanawake na katiba, uchaguzi na uongozi pamoja na mfuko wa wanawake wa Women Fund wanatizama uchaguzi huo.

Wadau hawa wanapoutizama uchaguzi ambao ni muhimu kwa demokrasia, wanawafunda viongozi wa serikali, taasisi zake, wanasiasa, wagombea na vyombo vya habari kutimiza wajibu wao kufanikisha uchaguzi.

Wanakumbusha kuwa ili uchaguzi uwe huru na haki na kumwezesha kila raia mwenye sifa kushiriki yanahitajika mazingira wezeshi na salama kwa wanawake na watu wenye changamoto za kimaumbile wakati wote wa uchaguzi. Katika mafunzo wanakumbusha wadau wote wa uchaguzi kuzingatie misingi ya ushindani wa haki na huru na usawa wa kijinsia kama ilivyoainishwa kwenye katiba, sheria, sera, mipango ya nchi na kubainisha kwenye mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo nchi imeridhia.

Jambo jingine TGNP Mtandao na wadau wengine, wanaisisitiza serikali kuhakikisha na kusimamia vyombo vya dola vilivyopewa dhamana ya kusimamia uchaguzi ili vizingatia miongozo na sheria zenye kulinda wanawake dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wakati wa uchaguzi.

Wanasisitiza kusimamia kuzingatia misingi ya usawa wakati wa uteuzi wa wagombea ili wanawake wateuliwe ndani ya vyama.

TGNP Mtandao wanakumbusha kusimamia matumizi ya fedha hususani ruzuku zitokanazo na kodi za wananchi ili zitumike kwa madhumuni ya kuziba mapengo ya jinsia na makundi mengine maalum wakati wa uchaguzi.

Aidha, wanakumbusha serikali kusimamia vyombo vya habari wakati wa uchaguzi ili vitoe fursa sawa kwa wagombea wa makundi yote wakati wa kampeni pamoja na kuvidhibiti visitumike kudhalilisha mgombea yeyote.

Kadhalika wadau hawa wanataka kuwe na usimamizi wa vyombo vya dola na taasisi zote zilizopewa dhamana ya kusimamia uchaguzi vinazingatia utawala bora na demokrasia shirikishi.

**TAASISI ZA SERIKALI**

Wanamtandao hao wanaanza na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kuisisitiza wakati wote wa uchaguzi kuwajibika ipasavyo kusimamia misingi ya haki, usawa, utawala bora katika kuteua wasimamizi wa uchaguzi na kubainisha mipaka na majimbo ya uchaguzi.

Wanaikumbusha NEC kusimamia na kuwajibika ipasavyo kutoa elimu ya uraia yenye kuzingatia misingi ya usawa katika makundi yote na demokrasia shirikishi.

Kwa upande wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, TGNP na Wanamtandao wanaikumbusha kutoa miongozo kwa vyama vya siasa yenye tafsiri ya kuviongoza kuzingatia haki za wagombea wa makundi yote, kusimamia na kutoa elimu ya uraia na mpiga kura inayozingatia haki za wagombea wote.

Kuhusu Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (Takukuru), angalizo kwao ni kumulika aina mbalimbli za rushwa zinazofanyika katika kipindi chote cha uchaguzi ikiwamo ngono ambayo pia imebainishwa kwenye kifungu cha 25 cha sheria namba 11 ya mwaka 2007 ya kuzuia na kupambana na rushwa wakati wa uchaguzi.

Neno kwa Jeshi la Polisi ni kuhakikisha linatambua jukumu lake kubwa la ulinzi wa raia wote na kuepukana na kutumia nguvu wakati wa uchaguzi.

Aidha, linakumbushwa kuepuka kuwabambikia raia makosa na kwamba pale penye ukiukwaji wa sheria au taratibu, kutumike busara ya kuelimisha au kuchukua hatua stahiki.

Kwa mahakama, wanamtandao wanaikumbusha kushughulikia kesi za uchaguzi kwa kutumia hekima ambayo haiendelezi ukiukwaji wa haki za wanawake, na watu wenye ulemavu.

Wanaikumbusha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), kusimamia kuzingatia haki makundi yote ya wagombea, wapiga kura na washiriki wote kuanzia mchakato wa kwanza wa shughuli hizo za uchaguzi mpaka mwisho.

**VYAMA VYA SIASA**

Wanamtandao hao wanavitaka kuwa na utaratibu wa kusimamia matumizi ya fedha hususani za ruzuku kutoka serikalini na kwamba pamoja na mambo mengine zitumike kupunguza mapengo ya jinsia ndani ya uongozi wa vyama na wakati wa uchaguzi.

Wanavitaka vyama kuweka mikakati ya kuwezesha wanawake na makundi maalum wakiwamo wenye ulemavu katika kampeni za uchaguzi.

Kuendesha siasa kwa kutumia nguvu za hoja na siyo nguvu za misuli, viwe na ajenda za kushawishi za kuviwezesha kushinda na siyo kutumia njia zisizo sahihi kujitafutia ushindi huo.

Wagombea, wanapewa rai ya kutambua wajibu wao katika kutekeleza azma ya uchaguzi ulio wa haki, huru na salama kwa kuhakikisha wanajielimisha taratibu zote za uchaguzi ikiwa ni pamoja na miongozo na sheria.

Kuhakikisha wanaendesha kampeni zilizo salama, kuheshimu haki za binadamu na wawe na uwezo wa kukemea vya rushwa.

Kwa vyombo vya habari, wanamtandao pamoja na kutambua kwamba, tasnia ya habari ina mchango mkubwa katika kufanikisha uchaguzi kwa kutoa taarifa sahihi hivyo vinatakiwa kuelimisha umma juu ya haki zao za ushiriki katika uchaguzi bila kusababisha athari zozote.

Rai kwa viongozi watakaochaguliwa, wanamtandao hao wanasema kwa viongozi watakaoaminiwa na kuchaguliwa na wananchi wanatakiwa wawajibike kutimiza ahadi zao za kujenga taifa la umoja wa kitaifa.

Kuimarisha utekelezwaji wa misingi ya usawa kama ilivyoainishwa kwenye katiba na katika mikataba ya kimataifa na kikanda kuhusu haki za makundi ya wananchi wote.

Aidha, kuboresha mikakati iliyopo na kubuni mipya ya kupunguza pengo la jinsia katika siasa, uchumi, na ustawi wa jamii.

Halikadhalika wanataka wawe na mikakati madhubuti itakayoainisha ni jinsi gani serikali inatambua mchango wa wastaafu na wazee walio katika sekta rasmi na zisizo rasmi.

Pia wanahimizwa kuweka mikakati ambayo itawahakikishia wanawake uhai wakati wanapojifungua, kwa kuwekwa katika mipango na vipaumbele vya taifa ili kupunguza vifo vya wajawazito, wazazi na watoto.

**MAKALA**

# RAHA YA DIGRII...

## •Kutafuta, kufanikisha fursa, kujiajiri si kusubiri zikufuate

**Na Gwamaka Alipipi**

"MIONGONI mwa sifa kinachojivunia Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam ni kutoa wahitimu wenye sifa 'wanaogombaniwa' katika soko la ajira. Kwa miaka 58 tangu kuanzishwa kwake, kimekuwa kikijivunia kutoa viongozi mbalimbali ndani na nje ya nchi." Anasema Mkuu wa Chuo Kikuu, Profesa Willium Anangisye.

Katika mahafali ya 49 yaliyofanyika Jumamosi iliyopita Novemba 16, mwaka huu, anawaasa wahitimu kuwa licha ya kuwa na sifa hizo,

wawe watu wa kutafuta fursa badala ya kusubiri ziwafuate.

Katika mahafali hayo wasomi 8,313 wakiwamo wanawake 3,201 sawa na asilimia 38.5 walihitimu katika ngazi mbalimbali.

Kati yao, wahitimu 95 walitunukiwa shahada za uzamivu, 575 shahada za umahiri, 250 stashahada za uzamili na 4,276 walitunukiwa shahada za awali.

Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Anangisye, anawahimiza wahitimu hao kuwa na hulka ya kuthubutu kujaribu mambo ambayo yanaonekana kuwa magumu wanapokuwa wakitekeleza wajibu wao wa kujitafutia maisha mazuri.

"Hata pale mtakaposhindwa kufikia mafanikio mliyotarajia, msife moyo, bali endeleeni kuwa na ari ya kujaribu tena na tena hadi mafanikio yapatikane," anasema Profesa Anangisye.

**NGUVUKAZI MPYA**

Profesa Anangisye anawakumbusha kuwa elimu waliyoipata, ni muhimu kujua kuwa ni sehemu ya nguvu kazi katika jamii, wepesi wa kujifunza mambo mapya na kuwa tayari kubadilika kwa haraka ili wasiachwe nyuma na ulimwengu.

"Ninawaasa pia mkadumishe sifa ya chuo chetu cha UDSM ambayo kimekuwa nayo tangu miaka ya 1960 ya kutoa watu mashuhuri waliochangia maendeleo ya nchi mbalimbali," anasema Prof. Anangisye.

Aidha, anasisitiza kuwa, wahitimu wa vyuo vikuu wanapaswa kuzingatia misingi ya kwenda na wakati katika kutekeleza kazi zao za kitaaluma watakazokuwa wanazifanya na vilevile katika maisha yao ya kila siku.

"Jitahidini kudumisha sifa ya chuo chetu hiki popote mtakapokuwa, kwa kuwa chachu ya maendeleo na mifano ya kuigwa na wengine. Kamwe msishushe hadhi ya chuo hiki kwa kufanya jambo lolote lisilofanana na sifa na umaarufu wake," anasema Profesa Anangisye.

Anawaasa wahitimu hao kwa kuwaeleza kuwataka wakumbuke kuwa wanao wajibu kwa UDSM na kwa taifa linalowategemea.

Anawaambia kwa UDSM chuo kimejizatiti katika kutoa elimu bora na yenye manufaa kwao na kwa vizazi vyao, huku kikiwawezesha kukabiliana na mabadiliko yanayoendelea nchini na duniani kwa ujumla.

"Kwanza kabisa narudia kutoa pongezi zetu za dhati kwenu kwa niaba ya uongozi na jumuiya nzima ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tunawapongeza kwa kutimiza vigezo stahiki vya kutunukiwa shahada katika fani na ngazi mbalimbali za uhitimu."



Wasomi kutoka UDSM waliohitumu katika fani mbalimbali hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**.

**MAENDELEO YA CHUO**

Akizungumzia maendeleo yaliyopatikana ndani ya mwaka mmoja katika chuo hicho, Prof. Anangisye alisema UDSM kitaanza kutoa mitihani ya kimataifa ya ujuzi wa lugha ya Kiswahili kuanzia Novemba mwaka huu.

Anasema UDSM imejenga ukuta wenye urefu wa mita 1,100 kuanzia mabweni ya Magufuli mpaka lango namba moja, lengo kuu likiwa ni kuimarisha ulinzi, usalama na amani chuoni hao.

Gharama za ujenzi ni Sh. milioni 635.348 zilizopatikana kutokana na vyanzo vya ndani vya mapato ya chuo.

Mafanikio mengine ni kuendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu nchini, yaliyofanyika katika mikoa 10 ikiwamo Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Lindi, Kaskazini Pemba, Katavi, Mbeya, Mwanza na Unguja Kusini, wanafunzi 1,800 walipatiwa mafunzo hayo.

Anataja mafanikio mengine kuwa ni kufanyika kwa Kongamano la Kimataifa la Vyombo vya Habari vya Kiswahili Duniani lililofanyika Mei 10, mwaka huu na kuwaleta pamoja wanataluma na watafiti kutoka katika nchi za Ulaya, Asia na Marekani.

**BARAZA LA CHUO**

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Baraza la UDSM, Jaji Damian Lubuva, anasema katika kukisimamia chuo na kuboresha utendaji, Baraza liliidhinisha sera na mapendekezo mbalimbali yakiwamo, sera ya mawasiliano ya UDSM, nyingine ni ya kupinga unyanyasaji wa kijinsia.

Wakati mapendekezo ni pamoja na la kuwa na Profesa Emeritus/Emerita, hawa ni wanataaluma wabebezi waliofika ngazi ya profesa au profesa mshiriki ambao wamestaafu kwa mujibu wa sheria lakini mchango wao bado unahitajika na chuo hicho.

Anasema jingine ni pendekezo la Taasisi ya Usimamizi wa Rasilimali za Madini kuwa Chuo Kiambata cha UDSM, ripoti ya mapendekezo ya uwekezaji katika ardhi ya UDSM.

**CHANGAMOTO**

Jaji Lubuva anasema Baraza la Chuo linatambua changamoto mbalimbali ambazo wafanyakazi wa chuo wanakutana nazo katika kutekeleza wajibu wao wa utoaji wa elimu bora.

"Kubwa ni uhaba wa wafanyakazi wanataaluma na waendeshaji, mikopo ya wanafunzi na uhaba wa malazi pia ni changamoto zinazoendelea kufanyiwa kazi na baraza. Bado tunaendelea kuiomba serikali isaidie katika utatuzi wa changamoto hizi".

Jaji Lubuva anawaambia washiriki kuwa masuala ya ulinzi na usalama kwa wanafunzi na wafanyakazi hususani kwenye mabweni na maeneo mengine ya chuo ni tatizo.

Anasema ipo mikakati imewekwa ya kuimarisha ulinzi na baadhi ya maeneo, kuwekewa taa za barabarani na ujenzi wa uzio.

"Kama baraza tunaendelea kuangalia ni namna gani tutaweka mikakati madhubuti zaidi ya kuimarisha usalama. Changamoto nyingine zinahusiana na kasi isiyoridhisha ya wahadhili kufanya utafiti na kuchapisha katika majarida ya kimataifa yenye hadhi inayokubalika," alisema Jaji Lubuva.

**WAHITIMU**

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wenzake, Arnold Matemu, mhitimu wa shahada ya awali katika elektroniki na mawasiliano, anataja kuhitimu kwao ni mwanzo wa hatua muhimu zaidi katika maisha yao na taifa kwa ujumla, kwani taifa linategemea mchango mkubwa kutoka kwao kutokana na elimu wanayopata.

Akizungumzia changamoto kama mhitimu kwa niaba ya wenzake, Matemu anasema UDSM bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile upungufu wa vifaa vya kujifunzia kwa vitendo kwenye kozi za sayansi, uhandisi na teknolojia.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 21 00)



**Dondoo: Kulia**

1. Mji wake mkuu ni Harare
7. Moyo 8. Makubaliano ya watu kwa maandishi
11.Dhihirishia kitu kilivyo
12.Chama cha Hitler
13.Aina ya fedha
14.Mke wa Raila Odinga
15.Chombo cha kuhifadhia maji
19.Msalani
21.Wingi wa Mtukutu
23.Samaki mkubwa wa umbo bapa na mkia mrefu 24.Fimbo
26.Ndara 27.Pata majeraha
28.Jahazi 29.Mti mgumu
30.Malizika

**Dondoo: Chini**

1. Kale 2. Jiji la miamba
3. Wajibu wa kutenda jambo
4. Daiana kwa watu waliokopeshana 5. Kikuku
6. Mila na desturi za watu
7. Lilongwe ni mji wake mkuu
9. Kwa utaratibu wake
10.Fuata amri 13. Sema asante
15.Mwiba wa mdudu
16.Nguo ndefu ya kike 17.Keti
18.Mojawapo ya nguzo tano za Uislamu 19. Ubinadamu
20.Tunda liotalo kwenye miiba
22.Sehemu ya kiwiliwili kati ya kifua na kinena
25.Motokaa

## Jibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| R | | G | H | A | R | A | M | A | | T | | S |
| A | C | H | A | M | A | | T | | C | H | A | I |
| S | | U | K | A | N | D | A | | | A | | K |
| I | | B | A | N | D | A | M | A | | M | T | I |
| | | A | | A | A | L | A | M | | A | | L |
| K | A | Y | A | | | I | | B | U | N | D | I |
| U | | A | | M | A | L | T | A | | I | | Z |
| N | A | B | I | I | | I | | T | | | | W |
| G | | A | | S | | | K | A | R | A | M | A |
| U | A | S | H | I | | J | | N | | M | | |
| R | | R | | N | Y | A | M | A | | A | | R |
| U | Z | A | | G | | N | | | | N | O | A |
| | | | M | I | T | I | H | A | N | I | | I |

# Serikali: Walemavu hawa bila ulinzi wanashirikije uchaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

WAKATI baadhi ya vyama vya siasa vipo kwenye kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji na vingine vikisuburi kuwaapisha viongozi wao, Chama cha Wasioona Tanzania (TLB), kina ombi maalumu kwa Jeshi la Polisi.

Kinalitaka kuwaandalia watu wenye ulemavu mazingira wezeshi ili washiriki kikamilifu katika kampeni, mikutano na masuala yote ya uchaguzi kwa uhuru na usalama ili kutimiza haki yao ya kikatiba.

Mratibu wa Idara ya Maendeleo ya Vijana, na Chipukizi TLB, Kiongo Itambu, anasema mazingira ya kampeni nyingi za kisiasa yamekuwa hayatoi fursa kwa watu wenye ulemavu kushiriki katika mikutano ya kampeni za kisiasa.

Anapozungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, anasema mazingira yaliyopo mpaka sasa ya namna ya kuendesha kampeni na michakato ya kisiasa ni kwa ajili ya watu wasio na ulemavu ambao wana maumbile timamu.

"Mara nyingi tunatamani kushiriki sana katika kampeni kusikia kile kinachosemwa au kuahidiwa na wagombea, na hata ikiwezekana kuwauliza maswali juu ya vipaumbele vya watu wenye ulemavu, lakini tunashindwa. Tukiogopa kukanyagwa au kuumizwa, hasa kunapotokea vurugu au msongamano mkubwa," anasema Itambu.

Anaongeza: "Mazingira ya kampeni yalivyo, hata kama nina mtu wa kunisindikiza akanipeleka nikasikilize hakuna tatizo, lakini shida inakuja pale kunapotokea vurugu au watu wengi wakaanza kusukumana. Inakuwa tatizo na hapa ni rahisi kunikanyaga, labda yule wa karibu yangu tu ambaye atakuwa ameniona nilivyo."

Kadhalika, anasema watu wenye ulemavu wamekuwa wakishindwa kushiriki katika kampeni kwa kuhofia usalama wao na kwamba imefika wakati serikali, na vyombo vya dola kuliangalia suala hilo na kuhakikisha kunawekwa mazingira ambayo yatasaidia kundi hilo nalo kushiriki katika kampeni hizo za uchaguzi kwa sababu ni haki yao ya kikatiba, kirakia na kimsingi.

"Mimi naamini jambo hili linawezekana, mamlaka husika zihakikishe kwamba kunapofanyika kampeni zozote kuwe kunatengwa eneo maalum ambalo kundi la wanaoishi na ulemavu watakusanyika lakini eneo hilo liwe na usalama wa kutosha na inapotokea vurugu wasiathirike," anaomba Itambu.

Anaongeza kuwa polisi iweke alama maalum ya kuonyesha eneo linalotumika kwa ajili ya kuketi watu wenye ulemavu kwa sababu, itasaidia kurahisisha wananchi wanaoshiriki katika kampeni hizo kulifahamu na kuepuka kuwakanyaga na kuwaumiza.



Watu wenye mahitaji maalumu wanahitaji mazingira wezeshi na usalama wakati wote ili washiriki katika kampeni na uchaguzi. **PICHA: MTANDAO**

Mratibu wa Idara ya Wanawake na Watoto na wa TPhicho, Rehema Hamis Darueshi, anasema watu wenye ulemavu wanasahaulika katika mambo mengi.

Anasema pamoja na kwamba hutamani kuwa sehemu ya washiriki katika shughuli mbalimbali ikiwamo za siasa ikiwamo kufika katika mikutano mbalimbali husussani za kampeni kama ilivyo kwa makundi mengine yasiyo na ulemavu, lakini hushindwa kutokana na mazingira yaliyopo wakihofia kuumia.

"Yaani pamoja na kwamba wakati mwingine tunajitahidi kujichanganya katika jamii ili angalau tusijisikie vibaya kutokana na hali tuliyonayo, lakini huwa inafikia hatua kuna mazingira yanatutenganisha kabisa na jamii, tunapambana na hali iliyojengeka katika jamii ya kukataliwa na kutengwa, lakini bado vita ni kubwa sana kushirikishwa," anasema Rehema.

Anasema kutokana na unyanyapaa uliopo katika jamii kwa kundi hilo, imechangia baadhi ya watu wenye ulemavu wenyewe kuanza kujinyanyapaa.

Anasema kutokana na hali hiyo, wamekuwa wakilazimika kuwapatia elimu juu ya uwezo na umuhimu wao wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii.

"Na ndiyo maana hata katika vipindi hivi vya uchaguzi tunakazana kusisitiza kwamba, tusiachwe nyuma. Tunaelekea katika kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa, watuandalie mazingira na sisi tushiriki katika kampeni hizo ili tufahamu tutaenda kupiga kura kwa watu wa namna gani," anasema Rehema.

Anaongeza: "Tunaamini kwamba hata namna wenye ulemavu wanavyojinyanyapaa wakati mwingine hata pale ambapo hawajanyanyapaliwa ni matokeo haya ya kuachwa nyuma katika mambo mbalimbali. Ifike mahali tulione kundi hili ni la muhimu na linatakiwa kushiriki katika kila kitu kinachofanyika katika nchi yao, mimi naamini hakuna jambo litakaloshindikana ni kujipanga tu.

Akizungumzia suala la ulinzi katika kipindi cha uchaguzi huo wa serikali za mitaa kwa upande wa makundi maalum, Mpelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI),

Robart Boaz, anasema Jeshi la Polisi linathamini sana kundi hilo na litaendelea kutoa ulinzi kwao kwa jambo lolote au shughuli yoyote ambalo kundi hilo litahitaji msaada wao kama linavyotekeleza kwa makundi yote.

"Ni kweli makundi ya watu wenye ulemavu, kinamama ni kati makundi ambayo

ni muhimu ambayo yanahitaji ulinzi wa hali ya juu, lakini niombe tu kwamba wanapokuwa na shughuli zao ambazo wanahitaji nguvu zaidi ya ulinzi au ulinzi maalum watutaarifu tu, sisi tupo tayari wakati wote kuwahudumia," anasema Boaz na kuongeza:

"Sisi upande wetu kazi yetu ni kuimarisha ulinzi na kuhakikisha usalama unakuwapo kwa makundi yote, kuhakikisha shughuli za kampeni na hata uchaguzi unafanyika kwa amani na utulivu pasipo mtu yeyote kupata madhara wala kutokea uharibifu wowote, tunaomba tushirikishwe kwa makundi haya na ikiwezekana kila mahali watakapokuwapo tufahamu na tujipange namna ya kuwalinda hata katika kampeni za uchaguzi."

Anasema ni vema wakaacha kuhofu juu ya usalama wao, badala yake washirikiane na jeshi hilo katika kuhakikisha kwamba wanapatiwa ulinzi maalum.

"Tunafahamu watu wenye ulemavu wako katika makundi tofauti na kila kundi huwa lina mahitaji tofauti ambayo ni maalum, kwa hiyo ni vema tukayatambua

makundi yao na tufahamu namna ya kujipanga katika kuwaimarishia ulinzi, kuna wenye ulemavu ambao hawaoni, ambao hawatembei na wengineo, tunaomba tushirikishwe, tuwatambue katika kuelekea kampeni za uchaguzi huu wa serikali za mitaa," alisema Boaz.

Katika mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu wa mwaka 2006 ambao Tanzania pia imeusaini, unaelezea namna ya kutambua kanuni na miongozo ya kisera iliyomo ndani ya mpango kazi wa dunia kuhusu watu wenye ulemavu na namna ya kuweka usawa wa fursa kwao katika kushawishi uendelezaji, utungaji na utathmini wa sera, mipango, programu na hatua mbalimbali katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kutoa fursa sawa kundi hilo.

Mkataba huo unazitaka nchi zilizouridhia, kutilia mkazo umuhimu wa kujumuisha masuala ya ulemavu kama sehemu ya lazima ya mikakati inayohusiana na maendeleo endelevu na kwamba ubaguzi dhidi ya mtu yeyote kwa msingi wa ulemavu ni uvunjaji wa hadhi ya asili na thamani ya nafsi ya binadamu.

## HABARI KIMATAIFA

# Muungano kuunda chama cha siasa

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

MUUNGANO unaotawala Ethiopia umeidhinisha kuundwa kwa chama kimoja cha kitaifa kutoka vyama vyake vinne vya kikabila, hatua inayokuja kuelekea uchaguzi mkuu wa 2020.

Ni juhudi za Waziri Mkuu Abiy Ahmed za kuleta mshikamano. Vyama vitatu kati ya vinne vinavyounda muungano wa Demokrasia ya Mapinduzi ya Watu wa Ethiopia, EPRDF, vimekubaliana kuunda chama kimoja cha kitaifa kuelekea uchaguzi utakaofanyika Mei mwakani.

Chama hicho kipya kitaitwa Prosperity Party. Hata hivyo, chama cha Tigrayan People's Liberation Front (TPLF) kilisusia makubaliano hayo na kusema hatua ya kuundwa chama kimoja cha kitaifa ni kama imeharakishwa na si ya kidemokrasia.

**Uamuzi wa makubaliano uliopitishwa wa vyama kuungana ni hatua muhimu ya kutumia nguvu zetu kufanya kazi kwa maono ya pamoja.**

Msemaji wake, Fekadu Tessema, viongozi wa vyama vitatu vinavyounda muungano waliidhinisha mpango wa chama kimoja. "Uamuzi wa makubaliano uliopitishwa wa vyama kuungana ni hatua muhimu ya kutumia nguvu zetu kufanya kazi kwa maono ya pamoja," alisema Waziri Mkuu Ahmed.

Kazi hiyo imedhihirisha ni jinsi gani taifa hilo la pili kwa idadi kubwa ya watu barani Afrika, lilivyogawika juu ya msukumo wa Waziri Mkuu wa kuiunganisha nchi na makundi tofauti ya kikabila ambayo yanatafuta uhuru zaidi.

Ahmed ana matumaini kwamba mageuzi yake ya haraka yanaweza kuwashawishi wapiga kura ambao wametengwa kwa miongo kadhaa ya dhuluma za tawala kabla ya uchaguzi wa mwakani.

Muungano wa Demokrasia ya Mapinduzi ya Watu wa Ethiopia EPRDF, ulianzisha mfumo wa kisiasa baada ya kutwaa madaraka mwaka 1991, ambayo yanatoa uhuru muhimu kwa mikoa tisa ya kikabila inayodhibiti kodi za ndani, elimu na majeshi yake ya usalama.

Watu wa Sidama walipiga kura ya maoni wiki hii ya kuamua iwapo waunde jimbo jipya la watu wa Sidama. Matokeo yake yanasubiriwa kwa hamu na yanaweza kuchochea makundi mengine ya kikabila kutaka uhuru zaidi.

Tume ya uchaguzi ya Ethiopia inatarajia kutangaza matokeo ya kura hiyo ya maoni leo Jumamosi. Hadi sasa Ethiopia imegawika katika majimbo tisa ambayo yana uhuru nusu huku kura ya maoni ya Sidama ikiweka uwezekano wa kuwapo na jimbo la 10.

Kura hiyo ya maoni iliyofanyika Jumatano wiki hii ilimalizika kwa amani. Waziri Mkuu Abiy Ahmed aliwashukuru watu wa Sidama kwa kupiga kura kwa amani. **DW**



Wajumbe wa muungano unaotawala Ethiopia wakiwa kwenye kikao jijini Addis Ababa. **PICHA:DW**

## Surua yaua 5,000 Congo

**KINSHASA,** Congo

TAKRIBAN watoto 5,000 wamefariki dunia nchini Congo kutokana na unaotajwa kuwa ni mlipuko mbaya zaidi wa surua duniani.

Ugonjwa huo maarufu kama ukambi umewaua takriban watoto 5,000 huko Congo mwaka huu 2019, baada ya ugonjwa huo kusambaa hadi mikoa yote. Takriban watoto 250,000 wameambukizwa mwaka ugonjwa huo, mwaka huu pekee.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema kuwa ugonjwa huo ndiyo janga linalosambaa kwa kasi mno.

Surua nchini Congo umeua idadi ilio mara mbili ya wagonjwa waliofariki kutokana na ugonjwa hatari wa ebola katika kipindi cha miezi 15 iliyopita. Surua ni virusi vinavyosababisha mtoto kuwa na mafua, homa kali, kutapika na kuharisha na kupungukiwa na maji. Siku chache baadaye mgonjwa anapata vipele mwili mzima ambavyo vinaanza usoni na kusambaa kote.

Wengi hupona, lakini surua inaweza kusababisha ulemavu wa muda mrefu. Inaweza kusababisha kifo hususan iwapo utasababisha homa ya mapafu (nimonia) au uvimbe ubongoni. **BBC**

# Waziri Mkuu Israel agoma kung'atuka

**JERUSALEM,** Israel

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamini Netanyahu, amegoma kuondoka madarakani baada ya kushtakiwa kwa tuhuma za kutoa hongo, kufanya udanganyifu na kuwavunja imani raia waliomchagua.

Netanyahu (pichani), alishtumu mashtaka hayo kama jaribio la mapinduzi dhidi yake. "Sitakubali uongo kushamiri", alisema katika hotuba ya kupinga kesi hiyo.

Alidaiwa kukubali kuchukua zawadi kutoka kwa wafanyabiashara matajiri na kutoa hongo ili aonekane kwenye vyombo vya habari mara kwa mara.

"Nitaendelea kuliongoza taifa hili, kulingana na sheria ya nchi," alitamba.

Katika hotuba yake ya dakika 15, Netanyahu alishutumu idara ya mahakama, maofisa wa polisi na wengine kwa kupanga njama dhidi yake wakiwa na nia yenye madai ya msukumo wa kisiasa.

"Katika mchakato huu mzima uliotiwa doa wachunguzi hawakuwa wakitafuta ukweli bali walikuwa wakinitafuta," alisema.

Aidha, aliwashutumu wachunguzi hao kwa kuwahonga mashahidi ili kusema uongo.

Awali Mwanasheria Mkuu, Avichai Mandelblit, alisema alitoa uamuzi huo kwa 'moyo mzito' lakini akasema imeonyesha kwamba hakuna asiyeweza kushtakiwa nchini Israel.

"Hatuna budi kufuata sheria sio suala la kisiasa," alisema Mandalbelt.

Tangazo hilo linajiri huku kukiwa na mkwamo wa kisiasa nchini Israel kufuatia



uchaguzi mkuu kufanyika mara mbili Aprili na Septemba.

Jumatano wiki hii, mpinzani wa Netanyahu Benny Gantz, alisema ameshindwa kubuni serikali ya muungano na walio wengi bungeni.

Alipewa fursa kujaribu baada ya Netanyahu kushindwa kufanya hivyo.

Rais Reuven Rivlin aliwaomba wabunge Alhamisi wiki hii kukubaliana kuhusu mtu atakayechukua wadhifa wa uwaziri mkuu katika kipindi cha siku 21 ili kuzuia kufanyika kwa uchaguzi mwengine wa tatu.

Baada ya mashtaka hayo kutangazwa, Gantz alichapisha ujumbe wa Twitter akimuunga mkono mwanasheria mkuu na maofisa wa polisi na kuandika 'ni siku ya kuhuzunisha'.

Maandamano pia yalifanyika dhidi ya Waziri Mkuu Netanyahu

Rais Reuven Rivlin aliwaomba wabunge siku ya Alhamisi kukubaliana kuhusu mtu atakayechukua wadhifa wa uwaziri mkuu katika kipindi cha siku 21 ili kuzuia kufanyika kwa uchaguzi mwengine wa tatu.

Baada ya mashtaka hayo kutangazwa, Gantz alichapisha ujumbe wa Twitter akimuunga mkono mwanasheria mkuu na maofisa wa polisi na kuandika 'ni siku ya kuhuzunisha'.

Mwanasheria Mkuu Mandelblit alisema Februari mwaka huu kuwa alilenga kumshtaki Netanyahu kwa kesi tatu tofauti zinazojulikana kama kesi 1,000, kesi 2,000 na kesi 4,000 .

Kesi ya 1000, anashtakiwa kulaghai na kuwavunja imani raia. Anadaiwa kupokea zawadi za mvinyo na sigara, kwa lengo la kumsaidia tajiri mmoja rafikiye.

Netanyahu anasema kwamba alipokea vitu hivyo kama zawadi ya kirafiki na kwamba hakumfanyia hisani yoyote, huku rafiki akikana kufanya makosa.

Kesi 2,000 ni mashtaka ya ulaghai na uvunjaji wa imani. Anadaiwa kukubaliana na mchapishaji wa gazeti moja kuweka sheria za kudhoofisha gazeti pinzani kwa lengo la kuangaziwa mara kwa mara na gazeti hilo. Mchapishaji huyo ameshtakiwa na mashtaka ya kutoa hongo.

Kesi 4000 ni madai makali na tuhuma za kutoa hongo pamoja na ulaghai na uvunjaji wa imani za wengi. Imedaiwa kwamba alipitisha maamuzi ambayo yalikuwa yakipendelea kampuni moja ya mawasiliano kwa lengo la kutangazwa mara kwa mara na vyombo vya habari. **BBC**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- 28

Mtunzi anapatikana (0716 350534)




Na Adam Fungamwango

NILIVYOPATA taarifa baadaye ni kwamba kuna baunsa mmoja alitumwa na mama hadi Tandale na kuja kuchunguza na kuuliza, hadi akapajua. Aliporudi kesho yake alichukua wenzake ndipo alipokuja kukukamata."

Edina alimtazama kwa makini Kadili ili kumuona amepokeaje taarifa hiyo.

"Wewe hukuhusika kabisa kuwatajia ninapoishi?"

"Kadili bwana, sasa mimi nimeshawahi kufika kwenu hata siku moja?"

"Basi kwa mawazo yangu mimi nilijua wewe ndiye uliyewaambia, na nikajua labda umelazimishwa."

"Nilazimishwe? Hata wangeniwekea kwenye tanuri la moto, nisingesema."

"Kwa nini?"

"Yaani nikusaliti wewe? Haiwezekani na haitowezekana. Nilikuomba mwenyewe tucheze muziki, ina maana mimi ndiye niliyekuwa na dhima ya kukulinda, ingekuwa ni dhambi kubwa kukuuza."

Kadili aligundua upendo mkubwa ndani ya moyo wa Edina."

"Enhee ikawaje?"

**Nilipokubali niliona sasa utaendelea kuwa hai mtu wangu, kwani tayari nimempumbaza mama, nikaolewa na Dk. Kapilima kwa sherehe kubwa sana kama binti wa kitajiri na ilipoisha nikaanza maisha ya mke na mume.**

"Nadhani yaliyotokea baada ya hapo wewe unayajua, nisingetaka kuyarudia kwa sababu yanaumiza, ukateswa na kudhalilishwa pale mbele ya kadamnasi ya wafanyakazi wa mama. Kama uliniona mimi nilikaa chini kabisa maana nilichukia na wala sikutaka kuongea kitu chochote."

"Ndiyo, nakumbuka marehemu mama yako, alisema kuwa wewe ulilia sana kunitetea, vinginevyo angeniua."

"Wala hakuongopa. Wanaoingizwa mle ndani kwa sababu za kukiuka maagizo, masharti yake hasa ya kibiashara, ya kibinafsi na sababu kama zako hivyo, huwa hawatoki salama, wanauawa na kuzikwa ndani mle mle. Mama yangu Kadili namjua mwenyewe, alikuwa ni mafia, alijuana na watu wengi wakubwa ambao wanamlinda. Angeweza kufanya chochote na akahonga, asichukuliwe hatua. Nilijua kabisa na wewe yakikukuta, utauawa. Nikalia na kumwambia mama kuwa kijana wa watu asifanyiwe lolote baya, akakataa.

Nikamwambia kama mtamuua Kadili basi na mimi nitachukua kisu na kujiua papo hapo.

Hili lilimtisha mama na siku ya pili akaniambia sitomuua, bali tutampa adhabu kidogo na kumuachia, nikaona heri nusu shari kuliko shari kamili, lakini nikawaambia adhabu mtakazotoa zisimwathiri kiafya, vinginevyo hakuna mtakachokuwa mmefanya ni sawa na kumuua tu."

Kadili alimtazama kwa makini Edina. Alitambua ndani yake kuna kitu zaidi ya upendo. Ni mtu ambaye amemsababishia matatizo bila kukusudia. Lakini akamtetea mbele ya mama yake na watumishi wake ambao nia yao ilikuwa ni kumpoteza duniani.

"Nashukuru sana Edina, nimerudi kukuchukulia kuwa wewe ni yule Edina wa zamani, yule yule niliyekutana naye disco."

"Kwani baadaye ulinichukuliaje?"

"Nilijua kwa kiasi fulani huenda na wewe unahusika, unajua nilikuwa najiuliza maswali mengi sana na yasiyo na majibu."

"Sijahusika na lolote lile na leo uko hai na uko hapa kwa sababu yangu."

"Ahsante sana bibie."

"Nashukuru na wewe pia."

Kadili alimtazama Edina kwa makini kama mtu ambaye alikuwa bado kuna kitu hakijaa sawa.

"Enhee, sasa ikawaje baada ya mimi kuachiwa, maana nikasikia umeolewa."

"Ndiyo, ni kwamba mama alitekeleza mpango wake, nikaolewa kwa nguvu na Dk. Deus Kapilima."

"Kwa nini hukukataa hadi unaolewa, baadaye unakuja kutoroka."

"Kadili nilikuwa nakataa, lakini baadaye kesi ikabadilika. Mama akakaa kikao cha siri na watu wake akawaambia kuwa kama nikiendelea kukataa, basi watatafuta mbinu zote ili wakuue wewe kwa sababu bado mama aliamini kuwa wewe ndiyo mtu wangu na mimi nakataa wanaume na nakataa kuolewa kwa sababu yako."

Kadili alishtuka. Edina mwenyewe aliona mshtuko wa Kadili ukiwa dhahiri. Alijua baada ya kuachiwa kwenye jumba jekundu alikuwa yuko salama. Alianza kuwa na mashaka ya usalama wake pale tu aliposikia Edina ametoroka kwa mumewe.

"Bado ulikuwa kwenye mahesabu ya mama na kundi lake, ilikuwa uuawe ama kwa ajali, sumu au kitu chochote kile, lakini isijulikane kama yeye ndiyo amesababisha kifo chako. Kingekuwa ni kifo ambacho hata mimi nisijue kuwa yeye amehusika kwa sababu kama ningejua ningelianzisha na kusingekalika, au na mimi ningekunywa sumu, kitu ambacho mama hakutaka kitokee.

Na kifo chako kiliandaliwa ili mimi niweze kukubali kuolewa kwa sababu mama aliamini kuwa wewe ndiye unayesababisha mimi nikatae mpango wake."

Kadili alibaki ameduwaa tu. Hakuna na nguvu za kusema neno lolote. Hakujua kuwa tangu alipotoka kwenye jumba jekundu alikuwa akitembea na kifo mkononi.

Na kwa mara nyingine tena, msababishaji ndiye aliyemuokoa.

"Kuna mtu wangu kati ya wafanyakazi wa mama ambaye kila kitu kikifanyika au kusemwa, ni lazima anipe taarifa za siri. Akaniambia jambo hilo. Kwanza niliwaza kuja kwako, nikutafute nikikupata nikuhamishe hapo ukakae sehemu nyingine, lakini nikaona nitaipa shida na wasiwasi familia yako.

Lakini pia hata huko unakokwenda mama alikuwa na mkono mrefu, ungeweza pia kujulikana. Nikaamua kuolewa ni kukunusuru, lakini nilikuwa na langu moyoni." Edina aliyasema maneno hayo kwa namna ya simanzi. Wakati Kadili akiwa kama amepigwa na shoti ya umeme, au kupigwa ganzi Edina aliendelea.

"Nilipokubali niliona sasa utaendelea kuwa hai mtu wangu, kwani tayari nimempumbaza mama, nikaolewa na Dk. Kapilima kwa sherehe kubwa sana kama binti wa kitajiri na ilipoisha nikaanza maisha ya mke na mume.

Kwa muda mfupi tu nilichokuja kugundua kuwa mimi nilikuwa simpendi, yeye alinipenda, lakini hakuwa mume mwema, utajiri wake na umaarufu ulimfanya kuendelea kumiliki wanawake wengi sehemu mbalimbali akiwa amejengea nyumba, kuwapangisha nyumba na vyumba pia. Anaweza akaondoka nyumbani wiki nzima akasema yuko kikazi. Mimi ni binti wa kitajiri. Nikamwajiri mpelelezi binafsi mmoja amchunguze kila anakokwenda na aniletee taarifa. Alikuwa na kila kitu hadi kamera. Wiki mbili tu akaniletea mrejesho.

Ilikuwa nusura nizimie.

Itaendelea Jumamosi

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

## VYETI VIMEPOTEA



**FITINA JOHN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.320/064** kilichotolewa na KIGOMA SEKONDARI mwaka 1993. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0131/0651** kilichotolewa na MAZENGO SEKONDARI mwaka 1996. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CHAT/RB/1356/2013.**

115530202

---

**JAMUHURU YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**FORM II**

**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**KATITKA MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 81/2019**

**OMBI LA HADIJA MOHAMED MUSTAPHA KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI MAREHEMU GAUDENCE ALOYCE MOSHI**

WATU WOTE WANAODAI KUWA NA MAHUSIANO WOWOTE NA MIRATHI YA MAREHEMU HUYO WANAALIKWA KUJANA KUHUDHURIA KESI WAKITAKA MNANO EHE 13-12-2019 KABLA YA MUOMBAJI KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI HIYO.
WOSA WA MAREHEMU HUYO UPO MAHAKAMANI WAWEZA KUKAGULIWA. TRH 22/11/2019

115530102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 163 YA 2019**

**BAINA YA**

**PETER CHAMHENE......................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ABDALLAH SONGORO....................MDAIWA**

**KWA: ABDALLAH SONGORO POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 11.12.2019 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**Anagalizo:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hayi ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 21/11/2019

115529702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Mahakama ya mwanzo CHAMWINO MJINI**
**wilaya ya DODOMA**

**MADAI NAMBARI: 692/2019**

**MDAI.......IMMARIKA FINANCIAL SERVICES**

**DHIDI YA**

**MDAIWA......................PETER SIMON MSIGWA**

**KWA...........................PETER SIMON MSIGWA**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA PESA **TSH.10,400,000/=**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatano tarehe 27/11/2019 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ya kukaitwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi* wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama* hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama* umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 19/11/2019.

115529802

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BALE ARUDI SPURS, ASEMA CALDERON




**MADRID,** Hispania

RAIS wa zamani wa Real Madrid, Ramon Calderon anaamini kwamba, kurudi kwa Gareth Bale katika klabu ya Tottenham Hotspur litakuwa jambo zuri zaidi na "suluhisho la kumaliza matatizo yake ya sasa" nchini Hispania.

Calderon anatarajia Bale mwenye umri wa miaka 30, atazomewa kwenye Uwanja wa Bernabeu baada ya staili ya kusherehekea wakati Wales ilipofuzu kucheza michuano ya Euro 2020, akiwa na bendera iliyoandikwa "Wales. Golf. Madrid." Ikiwa na maana kwamba Wales ya kwanza, Golf ya pili na Madrid ya mwisho.

Calderon amesema kama Bale alijua kilichoandikwa kwenye bendera hiyo ilikuwa ni "utoto".

Kurudi Spurs "ilitakuwa suluhisho kwa kila mmoja", aliongeza Calderon.

Kocha wa zamani wa Real, Jose Mourinho amechukua nafasi ya Mauricio Pochettino kuwa kocha wa Spurs na Calderon anaamini Bale anaweza kurudi London Kaskazini, ambako alikaa pale misimu sita kabla ya kuhamia Madrid kwa ada iliyoweka rekodi mwaka 2013.

"Ni kweli kwamba, Mourinho anamtaka mchezaji," amesema Calderon akiiambia BBC Redio Wales.

"Alisema hivyo mwaka 2017 wakati alipojaribu kumsajili yeye pale Manchester United na Real Madrid ikaamua kuongeza mkataba wake na Gareth Bale."

## Xhaka iga kwa Bellerin - Emery

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery amemshauri Granit Xhaka kujifunza kwa kuiga mfano kutoka kwa Hector Bellerin katika jitihada zake za kupata sapoti na mashabiki wa klabu hiyo.


Kiungo Xhaka anaweza kuwa kwenye kikosi kwa ajili ya mchezo wake wa kwanza baada ya siku nne wakati 'Washika Bunduki' hao wa London watakaposhuka dimbani kucheza na Southampton leo Jumamosi kwenye Uwanja wa Emirates.

Mchezaji huyo wa Uswisi hajacheza kwenye kikosi cha Emery tangu alipopokonywa unahodha baada ya kubwatukiana na mashabiki wa klabu hiyo wakati alipotolewa kwenye mchezo wa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Crystal Palace Oktoba 27, mwaka huu.

Emery sasa yupo kwenye harakati ya kukijenga kikosi ili kiwe na mahusiano chanya na mashabiki baada ya kuwa kwenye kitimoto kwa kushinda mchezo mmoja tu kati ya saba iliyopita kwenye mashindano yote.

Xhaka alibainisha kwamba kubwatukiana kwake na mashabiki ni kutokana na kukosa uvumilivu wa kutumiwa ujumbe wa vitisho kwenye mitandao ya kijamii na Emery amesema beki wa pembeni Bellerin pia alizungumza naye juu ya wakati wake mgumu alioutapa kutoka kwa mashabiki ambao walikuwa wakimshutumu.

Sasa, Emery anataka Xhaka kufuata mfano wa mchezaji mwenzake huyo wa kuweza kurudisha imani kwa mashabiki wa klabu hiyo.






## Rashford: Solskjaer ni bora kuliko Pochettino

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford amesisitiza kwamba hakuna kocha bora wa klabu hiyo kama Ole Gunnar Solskjaer licha ya taarifa kudai kwamba wanafikiria kumchukua Mauricio Pochettino.

Tottenham ilimfukuza Pochettino mapema wiki hii na nafasi yake ikachukuliwa na kocha wa zamani wa United, Jose Mourinho, huku Spurs wakiwa wameshinda mchezo mmoja tu kati ya minne kwenye mechi 18 za mashindano yote.

Kumekuwa na mazungumzo kwamba, United wanaweza kuangalia uwezekano wa kumchukua Pochettino ili achukue nafasi ya Solskjaer, ambaye ameweza kupata pointi zaidi ya mbili tu kuliko Spurs katika mechi 12 za ufunguzi wa msimu huu wa Ligi Kuu.

Hata hivyo, Rashford - ambaye alisaini miaka minne Julai mwaka huu - amesema mipango ya Solskjaer ilikuwa sehemu ya msimu huu na ndio sababu aliamua kukubali majukumu ya kuongeza mkataba.

"Sikuwa na muda wa kusitasita kwenye kusaini mkataba mpya," alisema akiiambia Sky Sports News.

"Na pia ilikuwa sawa na Ole - naweza kuona moyo wake uliko na anakotaka kwenda, ambako alitaka mimi kuwa sehemu ya klabu na mimi sikusita kabisa.

"Tulikuwa kwenye ukusara mmoja na alitaka mambo kuwa sawa. Ole ni mtu mzuri na moyo wake upo kwenye klabu hii, hivyo mimi naona hakuna mtu sahihi kwa kazi hii kama yeye katika klabu hii."

# Salah apigiwa upatu Misri Olimpiki 2020

**CAIRO,** Misri

KOCHA wa timu ya Taifa ya Misri chini ya umri wa miaka 23, Shawky Gharib, amesema ni mapema mno kutangaza maamuzi ya kumjumuisha mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, kwenye kikosi chake kwa ajili ya michuano ya Olimpiki 2020, itakayofanyika mjini Tokyo, Japan.

Tayari Misri imeshafuzu kushiriki michuano hiyo, kwa kutinga hatua ya fainali ya mashindano ya Afrika chini ya umri wa miaka 23, itakayofikia tamati kwa wenyeji kupambana dhidi ya Ivory Coast.

Kanuni za michuano ya Olimpiki zinatoa nafasi kwa kila timu shiriki kuwatumia wachezaji watatu waliozidi umri wa miaka 23, na tayari mashabiki wa soka nchini Misri wameanza kumshawishi kocha Gharib kutomsahau Mohamed Salah.

"Sina budi kujisifia kuwa sehemu ya Taifa la Misri, ninapendezwa na kila mchezaji mwenye uwezo wa kuichezea timu yangu, Salah ni mmoja wao, lakini ni mapema mno kusema kama nitamuita kikosini ama nitamuacha, tusubiri muda utakapofika nitafanya maamuzi," alisema Gharib.

"Natambua kila shabiki wa soka nchini hapa anataka kuona Mohamed Salah akiwa sehemu ya kikosi cha Misri kitakachokwenda Japan, lakini tukumbuke muda bado ni mrefu mno, tujipe nafasi."

Katika hatua nyingine mshambuliaji wa klabu ya Stoke City, Ramdan Sobhi, ambaye kwa sasa anaitumikia Al Ahly kwa mkopo, ameungana na mashabiki wa soka huko Misri kwa kusema, kuna haja ya kocha Gharib kumjumuisha Salah, kwenye kikosi kitakachoshiriki michuano ya Olimpiki 2020.





# MOURINHO: NINA FURAHA NA KIKOSI TOTTENHAM

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amesema anafuraha na kikosi alichokirithi kutoka kwa Mauricio Pochettino na amedokeza hatahitaji kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya usajili wa dirisha dogo Januari

Mourinho alitajwa kuwa kocha mpya wa Tottenham Jumatano, akichukua nafasi ya Pochettino, ikiwa ni kazi yake ya kwanza tangu alipofukuzwa Manchester United miezi 11 iliyopita.

Amerithi kikosi kinachojumuisha wachezaji, Christian Eriksen, Jan Vertonghen na Toby Alderweireld, ambao bado hawajasaini mkataba mpya na wanaweza kuondoka Spurs wakiwa wachezaji huru mwishoni mwa msimu.

Kulikuwa na uvumi wa kuwapo mgawanyiko kwenye vyumba vya kubadilishia nguo msimu huu chini ya Pochettino, lakini Mourinho amesisitiza alijaribu kuzungumza na wachezaji wote na "anajaribu kuwabakiza wachezaji bora na amekataa kuwaachia waondoke."

Wakati wa kipindi chake pale United, Mourinho alipata uzoefu wa wachezaji wakubwa kutoelewana nao akiwamo kiungo Paul Pogba, ambaye alionekana kutoelewana na Mreno huyo.

"Wachezaji... ni zawadi bora kwa kila kikosi," alisema Mourinho.

"Sihitaji wachezaji, nina furaha na wachezaji nilionao. Nahitaji muda tu wa kuwaelewa zaidi na najua kila kitu kipo sawa."

# *Maradona pasua kichwa, arudi kuinoa Gimnasia*

**BUENOS AIRES,** Argentina

DIEGO Maradona atabakia kuwa kocha mkuu wa klabu ya Gimnasia y Esgrima La Plata baada ya kubadilisha uamuzi wake wa kujiuzulu.

Mchezaji huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya Argentina na Napoli, alitangaza kujiuzulu Jumanne baada ya kushuhudiwa katika mechi nane ambapo alishinda tatu na kupoteza tano.


Maamuzi ya Maradona yalihusishwa na raia wa klabu hiyo ya Gimnasia, Gabriel Pellegrino, mtu ambaye alimshawishi kurudi kwenye kazi ya ukocha.

Hata hivyo, Maradona aliamua kubadilisha maamuzi wakati uchaguzi wa klabu hiyo ukitarajiwa kufanyika leo Jumamosi ambapo uliahirishwa kwa siku 15 akikubali kufanya kazi na klabu hiyo.

"Nina furaha kusema kwamba, bado nabakia kuwa mkuu wa benchi la ufundi la klabu ya Gimnasia ya Esgrima La Plata," aliandika Maradona kwenye ukurasa wake wa mitandao yake ya kijamii.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CEBALLOS NJE MWEZI, KOLASINAC NAYE SHIDA

**Presha kuongezeka kwa Emery leo akiivaa Southampton baada ya kuiongoza Arsenal...**

**LONDON,** England

KIUNGO wa Arsenal, Dani Ceballos anakabiliwa na kuwa nje ya kikosi kwa mwezi mzima kutokana na majeraha ya misuli.

Nyota huyo wa kimataifa wa Hispania alikumbwa na balaa hilo la kuumia wakati wakitoka sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Vitoria SC kwenye Europa League mwanzoni mwa mwezi huu.

Kocha Mkuu, Unai Emery mwanzo alichukulia kama "majeraha madogo" lakini, katika taarifa fupi iliyotumwa kwenye tovuti ya klabu hiyo kuhusu majeruhi waliyo nayo kikosini kuelekea mechi ya Ligi Kuu leo dhidi ya Southampton, Arsenal imethibitisha kuumia kwa Ceballos katika misuli ya mguu wa kushoto hiyo ikiwa maanisha kurejea kwake kamili kwenye mazoezi itakuwa katikati ya Desemba.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hadi sasa ameichezea Arsenal mechi 17 katika mashindano yote tangu atue hapo Uwanja wa Emirates kwa mkopo wa muda mrefu akitokea Real Madrid.**

Emery pia atalazimika kumtathmini kwanza Sead Kolasinac kabla ya mechi ya Southampton leo baada ya beki huyo wa kushoto kurudi katika majukumu ya klabu akiwa na majeraha ya misuli katika mguu wa kushoto.

Nyota huyo wa kimataifa wa Bosnia-Herzegovina, Kolasinac aliichezea nchi yake kwa dakika zote 90 wakati wakipokea kichapo cha mabao 3-0 dhidi ya Italia Ijumaa iliyopita.

Emery amejikuta mwenyewe katika presha kubwa kufuatia kuiongoza timu hiyo mechi nne za Ligi Kuu bila ushindi.

## ZISIKUPITE

### IBRAHIMOVIC KUSHTUKIZWA

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho anazingatia uwezekano wa kujaribu kuipiku AC Milan na kumsajili mshambuliaji nguli raia wa Sweden Zlatan Ibrahimovic, 38. ***(Telegraph)***

### LIVER KUMKOSA SALAH 2020-21

LIVERPOOL itamkosa winga wake wa kimataifa wa Misri, Mohamed Salah mwanzoni mwa msimu wa 2020-21 kufuatia nchi yake kufuzu michuano ya Olimpiki ambayo itafanyika Tokyo, Japan kuanzia Julai 24 hadi Agosti 9, mwakani. ***(Mirror)***

### DE LIGT AKANA MADAI KLUIVERT

BEKI wa Juventus na Uholanzi, Matthijs de Ligt, 20, amekana madai yaliyotolewa na mshambuliaji wa zamani, Patrick Kluivert kwamba anajutia kutua Italia akitokea Ajax majira ya joto. ***(Mirror)***

### PIQUE KUSTAAFU BARCA 2022

BEKI wa Hispania, Gerard Pique, 32, amesema atahitimisha soka lake hapo Barcelona mwaka 2022. ***(Mundo Deportivo)***

### MOURINHO AAHIDIWA BONASI

JOSE Mourinho atapokea bonasi ya pauni milioni mbili kama atafanikiwa kuiongoza Spurs kumaliza nafasi nne za juu msimu huu. ***(Sun)***

### POCHETTINO ATAKIWA BAYERN

KOCHA wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino anatakiwa na Bayern Munich kwenda kuinoa. ***(Sky Sports)***

### TORREIRA KUSEPA ARSENAL

KIUNGO wa Arsenal na Uruguay, Lucas Torreira, 23, hajaweka kando uwezekano wa kuachana na klabu hiyo Januari. ***(Sport 860 via Mirror)***

### P'GRINI, MOURINHO HAWASOMEKI

KOCHA wa West Ham, Manuel Pellegrini amesema Jose Mourinho si rafiki yake wala adui yake. ***(Talksport)***

### MATIC AWINDWA ATLETICO

ATLETICO Madrid imejiunga katika mbio moja na AC Milan katika kuiwania saini ya kiungo wa Manchester United, Mserbia Nemanja Matic, 31. ***(ESPN)***

### BARCA NAYO KWA POCHETTINO

BARCELONA pia inavutiwa na huduma ya kocha wa zamani wa Tottenham, Muargentina Mauricio Pochettino, 47 ambaye hivi karibuni aliwaongoza mahasimu wao, Espanyol. ***(Sun)***

### NEYMAR AMKERA TUCHEL

KOCHA wa Paris St-Germain, Thomas Tuchel amesema hakupenda kitendo cha mshambuliaji wa timu hiyo, Neymar kwenda Madrid kushuhudia Davis Cup. ***(Marca)***

### CUADRADO AJIFUNGA UPYA JUVE

KIUNGO Mcolombia Juan Cuadrado, 31, ametia saini mkataba mpya ambao utamuweka hapo Juventus hadi mwaka 2022. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

# HABARI MICHEZO

## MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Kagera Sugar | 11 | 7 | 2 | 2 | 16 | 9 | 23 |
| 2. Simba | 9 | 7 | 1 | 1 | 16 | 3 | 22 |
| 3. TZ Prisons | 12 | 4 | 8 | 0 | 14 | 9 | 20 |
| 4. Lipuli | 11 | 5 | 3 | 3 | 19 | 12 | 18 |
| 5. Alliance | 11 | 4 | 5 | 2 | 10 | 8 | 17 |
| 6. Polisi Tanzania | 10 | 5 | 1 | 4 | 11 | 8 | 16 |
| 7. Namungo | 11 | 5 | 1 | 5 | 10 | 11 | 16 |
| 8. Mtibwa Sugar | 11 | 4 | 3 | 4 | 10 | 11 | 15 |
| 9. Ruvu Shooting | 11 | 4 | 3 | 4 | 9 | 10 | 15 |
| 10. Coastal Union | 11 | 4 | 2 | 5 | 11 | 10 | 14 |
| 11. Mbao | 11 | 3 | 5 | 3 | 9 | 9 | 14 |
| 12. Yanga | 6 | 4 | 1 | 1 | 9 | 6 | 13 |
| 13. Azam | 7 | 4 | 1 | 2 | 7 | 4 | 13 |
| 14. JKT Tanzania | 10 | 3 | 3 | 4 | 8 | 10 | 12 |
| 15. Mwadui | 12 | 2 | 6 | 4 | 8 | 11 | 12 |
| 16. KMC | 9 | 2 | 2 | 5 | 6 | 10 | 8 |
| 17. Biashara Utd | 10 | 2 | 2 | 6 | 6 | 11 | 8 |
| 18. Mbeya City | 10 | 1 | 5 | 4 | 7 | 16 | 8 |
| 19. Ndanda | 10 | 1 | 4 | 5 | 6 | 11 | 7 |
| 20. Singida Utd | 11 | 0 | 4 | 7 | 4 | 15 | 4 |

# AUSSEMS BADO NJIAPANDA SIMBA, AACHIWA MAZINGIZA

**Na Shufaa Lyimo**

KAIMU Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Mwina Kaduguda 'Simba wa Yuda', ambaye ameteuliwa hivi karibuni baada ya aliyekuwa Mwenyekiti Swedi Mkwabi kuamua kujiuzulu, amesema bodi ya klabu hiyo itatoa maamuzi ya Kocha Mkuu, Mbelgiji Patrick Aussems kama ataendelea kuinoa ama laa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kaduguda alisema bodi hiyo imekutana na kuamua kwa pamoja kumuachia jukumu zima la kufanya uchunguzi wa kocha huyo, Mtendaji wao Mkuu, Senzo Mazingiza.

"Sisi huwa hatukurupuki bodi ilikutana juzi tukaamua kwa pamoja tumpe mtendaji mkuu jukumu la kuchunguza sakata zima la kocha akishatupa majibu bodi itakaa kwa mara nyingine na kutoa maamuzi ya mwisho," alisema Kaduguda.

**Aidha, alisema lengo lao ni kufanya mabadiliko makubwa ndani ya klabu hiyo, na kudai wana uwezo wa kumwajiri kocha kutoka nchi yoyote kutokana na Simba kuwa vizuri kiuchumi.**

"Sisi tuna pesa za kutosha, tuna uwezo wa kuchukua kocha kutoka nchi yoyote kwa sababu kifedha tuko vizuri na sisi hatutaki mpira wa maneno bali tunataka vitendo," alisema.

Alisema kocha amelewa sifa kutokana na mafanikio aliyoyapata ndani ya Simba na kusema wiki ijayo kila kitu kitawekwa hadharani kwani wanataka kufanya kazi na mtu mwenye weledi na nidhamu ya hali ya juu. Aliwataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kukaa na kusubiri kuona maamuzi ambayo yatatolewa hivi karibuni ili waweze kujua kile kinachoendelea ndani ya klabu hiyo.

Hayo yameibuka baada ya sintofahamu ya kocha huyo kuondoka kuelekea nchini Afrika Kusini huku yeye akidai alikwenda kwao Ubelgiji kwa matatizo binafsi.



Mshambuliaji wa Simba, Wilker da Silva (kulia), akishangilia na Mbrazil mwenzake Tairone Santos da Silva baada ya kuifungia bao timu yake kwa shuti kali wakati ikishinda 1-0 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya JKT Tanzania iliyopigwa Uwanja wa Chamazi Ijumaa iliyopita. **PICHA: MAKTABA**

# *Kilimanjaro Queens kuivaa Uganda kwa tahadhari leo*

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha timu ya soka ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens), kinatarajia kukutana na Uganda katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Kilimanjaro Queens ambao ni mabingwa watetezi wa michuano hiyo, wamefanikiwa kutinga hatua hiyo baada ya kushinda mechi zake zote tatu za Kundi A, huku Uganda ikimaliza ya pili kwenye Kundi B, ilishinda mechi mbili na kupoteza mchezo mmoja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Kilimanjaro Queens, Bakari Shime, alisema amekiandaa kikosi chake kucheza kwa umakini katika mchezo huo ili kufikia lengo lao ya kusonga mbele katika mashindano hayo yanayosimamiwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Shime alisema anajua mchezo huo utakuwa mgumu kutokana na wapinzani wao kujipanga kurekebisha makosa waliyoyafanya katika mechi yao ya mwisho dhidi ya Kenya ambayo walifungwa mabao 3-0.

"Haitakuwa mechi rahisi, kila timu inaingia uwanjani kupambana, timu zote nne zilizotinga hatua hii si mbaya, pia kumbuka sisi ni mabingwa watetezi na kila aliyefika hatua hii, anaweza kupambana kutwaa kombe la mashindano haya," alisema Shime.

Kocha huyo aliongeza kuwa hana majeruhi katika kikosi chake na ataingia uwanjani kwa tahadhari kwa sababu anafahamu wapinzani wao wameshawasoma wachezaji wake.

Naye Kocha Mkuu wa Uganda, Farida Bulega, alisema kuwa anatarajia kukutana na timu iliyojipanga, lakini anaahidi mchezo wa kiwango cha juu.

# Zanzibar Heroes yasimamisha ligi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imesimamisha mzunguko wa 11 wa Ligi Kuu Zanzibar Ili kupisha mazoezi ya timu ya Taifa (Zanzibar Heroes) yanayoendelea katika viwanja vya Mao na Amaan.

Akizungumza na gazeti hili, Katibu wa Kamati hiyo, Hussen Ahmada alisema ZFF imeamua kufanya hivyo baada ya kupokea barua kutoka kwa baadhi ya klabu za Ligi Kuu ambazo wachezaji wao zaidi ya wanne wamechaguliwa katika kikosi cha timu ya Taifa.

Alisema zipo baadhi ya klabu kama vile Malindi ambayo wachezaji wake sita wamechaguliwa katika timu ya Taifa na kwamba nyingine ni Mlandege, Zimamoto na KMKM.

Alisema kufanya hivyo pia kunampa nafasi Kocha Mkuu wa Zanzibar Heroes kuendelea na mazoezi pasipo kuathiri mwingiliano wa viwanja, ambapo Uwanja wa Amaan ulilazimika michezo ya ligi kuanza saa nane badala ya saa 10 jioni ili kutoa nafasi kwa timu hiyo ya taifa kufanya mazoezi yake kwa nyakati za jioni.

"Tulipokea barua kutoka kwa baadhi ya klabu za Ligi Kuu juu ya kuomba kusimamisha mzunguko huu kutokana na baadhi kudai wachezaji wao wanaowategemea kuchaguliwa katika timu ya Taifa, huku baadhi ya michezo ya mzunguko wa 10 Malindi na KMKM tulilazimika kuuweka kiporo," alisema

Aidha, alisema ligi hiyo ya Zanzibar itaendelea mzunguko wa 12 Novemba 30, 2019 na 11 utapangwa baadaye.

Michezo

Jumamosi Novemba 23, 2019

Nipashe



Ceballos nje mwezi, Kolasinac naye shida

UKURASA 30

MILIKI...



Winga wa Yanga, Jafari Mahammed (kulia), akimiliki mpira huku akizongwa na beki wa JKT Tanzania, katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba SC, Ruvu Shooting ni vita

**Na Somoe Ng'itu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanatarajia kuwakaribisha "Maafande" wa Ruvu Shooting kutoka Mlandizi mkoani, Pwani katika mchezo wa ligi hiyo utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kuwa wachezaji wake wamejiandaa kucheza katika kiwango bora kutokana na kufahamu upinzani unaonyeshwa na wachezaji wa Ruvu Shooting.

Rweyemamu alisema watacheza kwa tahadhari na umakini kwa sababu wanajua wapinzani wao wataingia na mipango ya kuhakikisha wanaondoka pia na matokeo mazuri katika mchezo huo.

"Tuko tayari kupambana kusaka ushindi, tumejiandaa vema na tumejipanga kuhakikisha tunafanya vizuri, tunajua hakuna mechi rahisi katika ligi msimu huu, ili ushinde, unatakiwa kuonyesha kiwango cha juu," alisema meneja huyo.

Aliongeza kuwa hawatawadharau wapinzani wao kutokana na namna walivyoimarika na wanavyopambana kupata ushindi katika kila mchezo wanaocheza.

"Ukiangalia mwenendo wao katika Ligi Kuu msimu huu ni mzuri, si Ruvu Shooting tu, kila timu tunayokutana nayo, utaona imejiimarisha kusaka ushindi, nasi tunapambana kuhakikisha hakuna kitakachoharibika, tunatumaini Mungu atatusaidia," alisema Rweyemamu.

Naye Ofisa Habari wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, aliliambia gazeti hili kuwa wamejipanga kuendeleza "ubabe" kwa timu kubwa za Dar es Salaam na huo mkakati utawafanya watimize malengo yao ya kumaliza kwenye nafasi za juu msimu huu.

Baada ya mechi za leo ligi hiyo itasimama tena kupisha timu ya Taifa ya Tanzania Bara kujiandaa na mashindano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 7, mwaka huu jijini Kampala, Uganda.

# Yanga ni mchakamchaka, Simba yashushwa kileleni

**Na Adam Fungamwangwo**

### ●●● Molinga, Sibomana, Balinya wafanya kweli huku Kagera Sugar sasa ikikalia usukani...

MABINGWA watetezi wa soka Tanzania Bara Simba wameshushwa kileleni, huku watani zao wa jadi Yanga wakiichapa JKT Tanzania mabao 3-2 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam na kukwea hadi nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Simba imeng'olewa kileleni baada ya Kagera Sugar kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Lipuli kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, hivyo kufikisha pointi 23 kwa mechi 11 ilizocheza na kuwaacha 'Wekundu wa Msimbazi' hao wakiwa na pointi 22 kwa mechi tisa walizocheza, huku Jumamosi wakiwa na mechi dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Ligi Kuu Tanzania Bara imeweka rekodi ya aina yake, baada ya mabao matano kufungwa kipindi cha kwanza kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana, Yanga ikiifunga JKT Tanzania mabao 3-2.

**Mapema tu dakika ya 11, Patrick Sibomana alipopachika bao la kwanza kabla ya straika hatari aliyekuwa akiichachafya ngome ya Yanga, Adam Adam kusawazisha dakika mbili baadaye, ikiwa ni bao lake la tatu msimu huu akiwa na klabu hiyo.**

Juma Balinya aliipatia Yanga bao la pili dakika ya 21, baada ya uzembe wa mabeki wa JKT Tanzania kukosea kuuondoa mpira kwenye eneo la hatari na straika David Molinga alifunga bao la tatu kwa mkwaju wa faulo dakika ya 35 na kuwa lake la tatu kwenye Ligi Kuu msimu huu. Dakika moja kabla ya mapumziko, Danny Lyanga aliipatia JKT Tanzania bao la pili, baada ya kuwatoroka mabeki wa Yanga na kuunganisha krosi ya Adam.

Kipindi cha pili timu zote zilitulia baada ya kufanya mabadiliko na kufanyia kazi makosa ya kipindi cha kwanza, hivyo kusababisha kutokuwa na mwanya wowote wa timu kuongeza bao.Yanga imepanda hadi nafasi ya 12 kwenye msimamo kwa kuwa na pointi 13, kwa mechi sita ambazo imecheza mpaka sasa, wakati JKT Tanzania ikiwa nafasi ya 14 na alama 12 baada ya kushuka dimbani mara 10.

Kwenye Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi, kwa mara ya kwanza Namungo FC imeonja shubiri nyumbani kwa kuchapwa mabao 3-1 dhidi ya Coastal Union ya Tanga, Alliance ikiwa nyumbani Uwanja wa Nyamagana mjini Mwanza imepata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya KMC ambayo inazidi kudidimia, Ndanda FC nayo ikiwa nyumbani Nangwanda Sijaona mjini Mtwara imekiona cha moto kwa kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Polisi Tanzania, huku Prisons ikilazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani Uwanja wa Sokoine dhidi ya Mwadui FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >